# Nipashe

Jumamosi Oktoba 17, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580371

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710





UKURASA 11

**LISSU** asisitiza kura uchaguzi 2020 ina umuhimu wa kipekee



UKURASA 3

**VIONGOZI** wa dini wawaasa vijana uvunjifu wa amani

UKURASA 2

# BAKWATA yakunjua makucha

**YAWAONYA** viongozi wake kushiriki kampeni za vyama vya siasa... *Endelea Uk. 2*



Sheikh Mkuu wa Tanzania, Abubakar Zuberi

## Tume ya Amani, Maalim Seif wateta saa moja

UKURASA 3



Mgombea wa urais wa Zanzibar kupitia ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, nyumbani kwake Chukwani, nje kidogo ya Mji wa Zanizibar jana, baada ya kumaliza kikao na Kamati ya Amani ya Kitaifa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**


## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

**WASAIDIZI WA MAJAJI WAONYWA KUHUSU SIASA**

JAJI Mkuu mstaafu wa Tanzania, Mohamed Chande Othman, amewataka wasaidizi wa sheria wa majaji...

**UKURASA WA 4**

**WAKILI MKUU SERIKALI AOKOA TRILIONI 11.4/-**

OFISI ya Wakili Mkuu wa Serikali, imeokoa Sh. trilioni 11.4 baada ya kushinda kesi...

**UKURASA WA 8**

**KISHIMBA AIBUKA NA MBINU MPYA KAMPENI**

MGOMBEA ubunge wa Kahama Mjini, Jumanne Kishimba (CCM), ameibuka...

**Kamati Maadili yamwonya mgombea CHADEMA**

UKURASA 2

**MICHEZO** KAZE KUISUKA YANGA KISASA UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**



**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

# Kamati ya Maadili yaonya mgombea ubunge CHADEMA

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

KAMATI ya Maadili ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi Jimbo la Shinyanga Mjini, imempa onyo mgombea ubunge wa jimbo hilo, Salome Makamba (CHADEMA), kuhusu madai ya uzushi aliyotoa dhidi ya mgombea mwenzake wa CCM, Partobas Katambi.

Samole anadaiwa kumzushia Katambi kuwa amekuwa akikashifu wanawake kwenye mikutano yake ya kampeni, lakini alipotakiwa kutoa ushahidi wa madai hayo, alishindwa.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo Jimbo la Shinyanga Mjini, Geoffrey Mwangulumbi, alisema jana kuwa Salome amepewa onyo hilo baada ya kushindwa kutoa ushahidi kuhusu kashfa hiyo.

"Tulipokea malalamiko kutoka kwa mgombea ubunge wa CCM Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, kwamba mgombea mwezake, Salome Makamba, anamchafua kwa kumzushia kuwa anawakashifu wanawake kuwa hawezi kushindana na mwanamke ayekwenda hedhi kila mwezi.

"Baada ya kusikiliza malalamiko hayo ya Katambi, tulimwita Salome ili atuthibitishie madai yake, akasema ushahidi anao, lakini siku tuliyomtaka alete ushahidi akashindwa ndipo tukampa onyo," alisema.

Alisema kama kuna mgombea ambaye hajaridhika na uamuzi uliotolewa, anaruhusiwa kwenda kushtaki kwenye ngazi za juu zaidi.

Kwa upande wake, Salome alipotafutwa kuzungumzia uamuzi huo, alisema anatii na kuyaheshimu maagizo yaliyotolewa na kamati hiyo.

# BAKWATA yakunjua makucha

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Ulamaa BAKWATA Taifa, limewazuia viongozi wake kufanya kampeni hasa katika majumba ya ibada kwa chama chochote cha siasa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Katibu wa baraza hilo, Sheikh Hassan Chizenga, viongozi wao wametakiwa wawe walezi wa jamii wanaopaswa kuwa kimbilio la umma.

"Baraza chini ya uenyekiti wa Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir, limekubaliana haya kupitia kikao chake cha dharura kilichokaa Oktoba 15 kuhusu yanayojitokeza katika kampeni za uchaguzi mkuu na kuhusisha dini ya Kiislamu," alisema.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa baraza limewasihi viongozi hao kubaki kuwa wasuluhishi, wapatanishi na walezi wa jamii inayowahusisha wafuasi wa vyama na wasio wa vyama.

Baraza hilo pia limewakumbusha viongozi hao na waislamu wote kuwa dua katika uislamu ni ibada na lazima ifanywe kwa mujibu wa mafundisho ya dini na siyo vinginevyo.

"Kauli ya dua yoyote yenye kwenda kinyume cha mafundisho ya uislamu itakayofanywa na kiongozi yeyote wa baraza, kamwe isihusishwe na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA)," ilibainisha taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema kuwa, baraza linawataka waislamu na Watanzania kwa ujumla kuendelea kuiombea nchi ili uchaguzi mkuu ufanyike salama na kwa amani.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (kushoto), akiangalia samaki aina ya jodari aliyeshikiliwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, alipotembelea mabanda ya wizara hiyo, kwenye maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani, yaliyofanyika kitaifa mkoani Njombe jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Viongozi wa dini waasa vurugu uchaguzi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

VIONGOZI wa dini mkoa wa Dodoma, wamewataka vijana kuacha kufikiria kufanya vurugu katika uchaguzi mkuu, badala yake wahimizane kutunza amani iliyopo.

Rai hiyo ilitolewa jana na Askofu wa Kanisa la Evangelistic Assemblies of God Tanzania (EAGT) Jimbo la Dodoma, Evans Chande, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Kiongozi huyo alisema wameamua kutoa angalizo hilo baada ya kuona kuna viashiria vya kuhamasisha vurugu kwenye uchaguzi huo uliopangwa kufanyika Oktoba 18, mwaka huu.

"Sisi viongozi wa dini tunawaasa vijana kwa pamoja bila kujali itikadi zao wakatae kutumiwa na maadui zetu wasioitakia mema nchi yetu, na tumkatae mgombea ambaye anashawishi vurugu," alisema Askofu Chande.

Aidha, aliwataka Watanzania kuwachagua wagombea wanaohubiri amani na maendeleo ya nchi ya Tanzania na si vinginevyo.

Askofu Chande alisema maandamano na vurugu si njia sahihi ya kudai haki bali watu wanatakiwa kutii sheria pindi wanazipodai.

Chande alisema endapo vurugu zitatokea, waathirika wakubwa yatakuwa makundi ya watoto, walemavu, wanawake na wagonjwa.

Pia alisema kila kwenye haki ya kupiga kura ajitokeze siku ya uchaguzi kuchagua viongozi wachapa kazi watakaoipeleka mbele nchi kimaendeleo.

Naye Katibu wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Dodoma, Sheikh Hussein Kuzungu, aliwataka Watanzania waangalie mifano katika nchi zilizoingia machafuko kwa kuhamasisha kufanya vurugu ambazo zimesababisha kuzorotesha maendeleo.

Sheikh Kuzungu alisema viongozi wa dini wanafuatilia taarifa hizo ambazo zinasambazwa kwa njia ya mitandao, simu watakapomaliza kazi yao wataweka hadharani majina ya wahusika kwa maslahi ya taifa.

Alisema kuna maisha baada ya uchaguzi hivyo watu wasidanganyike na maneno ya wagombea wanaotumiwa kuleta vurugu nchini.

HABARI KITAIFA

# Kamati ya Amani, Maalim Seif wateta kwa saa moja

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI ya Amani ya Kitaifa Zanzibar imekutana na mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT- Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, na kukubaliana kukutana tena ili kuzungumzia umuhimu wa amani.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Salum Muhammed, ndiye aliyeongoza mazungumzo hayo yaliyodumu kwa takriban saa moja, akiwa na wajumbe wake yaliyofanyika nyumbani kwa Maalim Seif, Chukwani mjini Zanzibar.

Salum alisema kamati hiyo imeamua kukutana na wagombea wa nafasi ya urais wa Zanzibar na wadau wengine wakiwamo viongozi ili kuwakumbusha umuhimu wa kuzingatia amani wakati wa kampeni, kabla na baada ya uchaguzi mkuu.

"Suala la amani lina umuhimu mkubwa tumebadilishana mawazo kuhusu mambo mengi na tumefikia mahala pazuri, lakini tumekubaliana upo umuhimu wa kuendelea kukukutana kuelekea uchaguzi mkuu," alisema.

Alisema kikao kama hicho kiliwahi kufanyika mwaka 2015 na wameona upo umuhimu wa kukutana tena katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, ili kusisitiza umuhimu wa amani kwa maslahi ya wananchi na taifa.

Kwa upande wake, Maalim Seif alisema hakuna amani bila ya haki na aliwataka viongozi na watendaji wenye dhamana ya uchaguzi kuhakikisha wanaheshimu haki ili kudumisha amani.

Maalim Seif alisema baada ya kupokea barua ya ombi la kukutana na kamati hiyo, alitafakari na kutoa uamuzi wa haraka ya kukutana na kamati nayo huku akiwataka kuendeleza utaratibu wa kufanya vikao kama hivyo vya kubadilisha mawazo na kukumbusha umuhimu wa amani kwa maslahi ya Zanzibar.

"Jambo la msingi huwezi kuwa na amani bila ya haki hivyo jambo la msingi tuzingatie kusimamia haki wakati tunaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu," alisema Maalim Seif.

Viongozi wengine wanaounda kamati hiyo kutoka madhehebu mbalimbali ya dini ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Askofu Michael Hafidhi wa Kanisa la Aglikana Dayosisi ya Zanzibar, Katibu wa Kamati Sheikh Fadhil Suraga na wajumbe kutoka Kanisa Katoliki na kiongozi wa Hindu na Masai.




Mgombea mwenza wa kiti cha urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salum Mwalimu, akihutubia mkutano wa kampeni katika Jimbo la Mpanda, mkoani Katavi juzi. **PICHA: FRANCIS DANDE**

# Tundu Lissu: Kura yako mwaka huu ni muhimu

**Na Romana Mallya**

MGOMBEA urais, Tundu Lissu (CHADEMA), amesema wananchi wanapaswa kutambua kura watakayopiga Oktoba 28 mwaka huu, ni muhimu kuliko yoyote waliyowahi kupiga katika uchaguzi mkuu.

Lissu alitoa kauli hiyo jana wakati akihutubia wananchi waliojitokeza katika mkutano wake wa kampeni uliofanyika Meatu mkoani Simiyu.

Alidai kwa mara ya kwanza tangu waingie kwenye mfumo wa vyama vingi, mwaka huu Chama Cha Mapinduzi (CCM) anaona kinaondoka madarakani.

"CCM lazima iondoke, nimepita karibu nchi zima kuzungumza na wananchi, wapo tayari kuondoa, msiwe na wasiwasi, ajenda kuu za uchaguzi mwaka huu zipo tatu; kurudisha uhuru wa wananchi, tunazungumza haki na maendeleo," alisema.

Akiwa Urambo mkoani Tabora, Lissu alisema kuwa akipata ridhaa ya urais, atatengeneza katiba mpya itakayorudisha mamlaka na rasilimali kwa wananchi ili kuondokana na hali ya kuwa ombaomba.

"Hakuna kitu kibaya kama watu wazima tunaondesha familia kila mahali kila mtu kuwa ombaomba, turudishiwe mamlaka, tuamue mambo yetu, ndivyo wanavyofanya nchi zote zinazoendelea," alisema.

Lissu alisema namna pekee ya kuondokana na utaratibu huu ni kutumia kura Oktoba 28 mwaka huu kwa kumchagua.

# Wasaidizi wa majaji waonywa kuhusu siasa

**Na Mwandishi Wetu,**
LUSHOTO

JAJI Mkuu mstaafu wa Tanzania, Mohamed Chande Othman, amewataka wasaidizi wa sheria wa majaji kutumia taaluma yao na kuzingatia umahiri na weledi katika uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi sambamba na kujiepusha na ushabiki wa kisiasa.

Alisema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya wasaidizi wa sheria 39 wa majaji wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu ya Tanzania juu ya namna uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi yaliyofanyika katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama (IJA) Lushoto, mkoani Tanga.

Chande aliwaomba washiriki hao kuzingatia na kufuatilia mafunzo hayo kikamilifu ili wakayatumie katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Mkiwa wasaidizi wa sheria wa majaji, ni vyema kutumia taaluma yenu vizuri na kuzingatia umahiri na weledi katika uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi na kujiepusha na ushabiki wa kisiasa," alisema.

Pia aliwataka washiriki hao kufanya kazi kwa kuzingatia maadili, umakini na kujiamini katika uandishi wa hukumu hivyo wanalazimika kuendelea kujinoa ili kuendana na kasi ya mabadiliko na izingatiwe kuwa wao ni msaada mkubwa kwa majaji katika utekelezaji wa majukumu ya utoaji wa haki.

Katika hatua nyingine, Jaji Chande aliupongeza Uongozi wa Mahakama ya Tanzania na wa IJA kwa kuwa mstari mbele katika kufanikisha mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa mbalimbali wa mahakama katika kushughulikia mashauri ya uchaguzi.

Mpaka sasa, mahakama kwa kushirikiana na IJA imeshafanya mafunzo ya uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi kwa maofisa mbalimbali wa mahakama.

Miongoni mwa maofisa walionufaika na mafunzo hayo ni majaji wa Mahakama ya Rufani, majaji wa Mahakama Kuu, naibu wasajili na mahakimu wakazi wafawidhi lengo likiwa kuwawezesha kuyashughulikia kwa ustadi zaidi na kwa wakati.

# Askofu ahimiza usomaji vitabu

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mara, George Okoth, amewataka vijana, wanafunzi na jamii kwa ujumla kujenga tabia ya kuingia maktaba na kusoma vitabu mbalimbali, ili kuongeza maarifa.

Wito huo aliutoa jana wakati akipokea jengo la maktaba lililojengwa katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya ACT-Bunda, inayomilikiwa na kanisa hilo.

Alisema wanafunzi na jamii nzima kwa ujumla wakijenga tabia ya kusoma vitabu mara kwa mara, watapata uelewa wa hali ya juu na kuongeza maarifa jambo ambalo litawasaidia katika maisha yao.

"Ninatoa wito kwa wanafunzi na wanajamii nzima kwa ujumla kujenga tabia ya kusoma vitabu, ili kujiongezea maarifa zaidi," alisema Askofu Okoth.

Askofu huyo aliipongeza kampuni ya ujenzi ya Mrefu iliyojenga jengo hilo kwa kufanya kazi kwa uaminifu na kuongeza kuwa ataendelea kuitumia kwa kuwa inajenga majengo kwa kiwango kinachotakiwa.

Katibu Mkuu wa Anglikana Dayosisi ya Mara, Maximilian Lyamsema, pamoja na Mkurugenzi wa Elimu, Arthur Mauya, walisema maktaba hiyo itakuwa na vitabu vya aina mbalimbali pamoja na vifaa vya kila aina ambavyo ni vya kisasa.

Viongozi hao pia walitoa wito kwa wafanyakazi wote wa shule hiyo kujenga tabia ya kusoma vitabu katika maktaba hiyo.

"Si kwamba ni kwa ajili ya wanafunzi tu hata nyie walimu na wafanyakazi wote mlioko katika shule hii, mtakuwa mnasoma vitabu katika maktaba hii," alisema Lyamsema.

Mhandisi wa kampuni ya Mrefu, Elias Leonard, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Kulwa Kahabi, walisema jengo hilo lina ubora unaotakiwa, huku Makamu Mkuu wa Shule hiyo, Godfrey Erasto, akilishukuru kanisa kwa kuwajengea maktaba hiyo.

"Tunashukuru sana kanisa hili kutupatia ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na sisi tunatekeleza kwa uaminifu mkubwa," alisema Mhandisi Leonard.

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo walisema maktaba hiyo itawasaidia kuongeza maarifa zaidi.

# Wakili mkuu serikali aokoa trl. 11.4/-

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

OFISI ya Wakili Mkuu wa Serikali, imeokoa Sh. trilioni 11.4 baada ya kushinda kesi za nje na ndani ya nchi ambazo zilikuwa zinaikabili serikali kwa kipindi cha mwaka 2019/20.

Pia ofisi hiyo imeshinda mashauri ya kuzuiwa kwa mali za serikali ikiwamo ndege zilizokuwa zimekamatwa Afrika Kusini na Canada.

Wakili Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata, aliyasema hayo jana kwenye semina ya kuwajengea uwezo mawakili wa serikali katika utendaji kazi wao iliofanyika jijini hapa. Alisema ofisi hiyo ilianzishwa kwa ajili ya uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi.

"Ofisi hii inawajibika kila siku kwa mashauri yaliyofunguliwa dhidi ya serikali na ilianza kazi mwaka 2018. Katika mwaka wa fedha 2019/20 ulioishia Juni, mwaka huu, imeokoa Sh. trilioni 11.4 kutokana na mashauri yaliyohusisha fedha yaliyokuwa yamefunguliwa ndani na nje ya nchi," alisema. Pia alisema kuna mali za serikali zilikuwa zimekamatwa nje ya nchi zikiwamo ndege zilizokamatwa Afrika Kusini na Canada na kupitia ofisi hiyo, serikali iliendesha mashauri na mali hizo kuachiwa baada ya kushinda kesi.

Malata pia alisema ofisi hiyo imerejesha serikalini mashamba 106 ambayo yalikuwa yametwaliwa na watu wenye nia mbaya dhidi ya mali za serikali.

"Vile vile kuna viwanja, hoteli na nyumba mbalimbali ambazo zilikuwa zimetwaliwa na watu wasio na nia njema na serikali nazo zimerejeshwa ikiwamo Hoteli ya Mbeya na iko mikononi kwa Shirika la Reli Tanzania," alisema.

Hata hivyo, alisema kutokana na mafanikio, wameona ni vyema kuendelea kuwajengea uwezo mawakili ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

"Mafunzo haya yameandaliwa ili kuwaongezea ujuzi katika maeneo mbalimbali baadhi ya maeneo ni ustadi wa ukusanyaji wa maelezo na kuandaa kesi, stadi za kuandaa hati na utetezi, uandishi wa maelezo na ushahidi, kuongeza mashahidi kutoa ushahidi mahakamani, ushahidi wa kielektroniki, wajibu wa mawakili kwa serikali na mahakama, jamii kwa ujumla," alisema.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Amon Mpanju, alisema serikali inaamini mafunzo hayo yataleta manufaa makubwa kwenye utendaji kazi wao.

Aliwataka mawakili kuhoji wakufunzi pale ambapo hawajaelewa ili kuongeza ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.



Mwenyekiti wa jumuiya ya watu wenye ulemavu wa CCM, Peter Sarungi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wakiipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kwa kuwapa kipaumbele watu wenye ulemavu kwa kutokupanga foleni siku ya kupiga kura katika uchaguzi mkuu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Siri kushamiri ukatili yatajwa

**Na Sabato Kasika**

HOFU ya kuachwa na kutojiamini, ni miongoni mwa sababu zinazotajwa kuwa chanzo cha wanawake kuendelea kuvumilia ukatili wa kijinsia kwenye ndoa bila kuchukua hatua.

Mbali na sababu hizo, sababu nyingine zinazotajwa kuchangia hali hiyo ni hofu ya aibu katika jamii, hofu ya ukahaba wakiachika na pia kulinda siri za familia.

Mwezeshaji katika semina ya walezi wa klabu za jinsia, Beatrice Ezekiel, alibainisha hayo juzi jijini Dar es Salaam, akiwataka wanawake kuchukua hatua za kutoa taarifa za ukatili wanaofanyiwa kwenye vyombo husika ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Semina hiyo iliandaliwa na Jukwaa la Vijana Wanaharakati (YFF) kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa kushirikiaha walezi wa klabu za jinsia katika shule za msingi na sekondari.

"Zipo sababu nyingine za wanawake kuwa hivyo, ikiwamo kutofahamu sheria zilizopo, mshikamano uliopo katika familia, hofu ya mtazamo wa watu na hofu ya usalama na utegemezi wa kiuchumi," alisema Beatrice.

Mwezeshaji huyo alisema wanawake wanaofanyia vitendo hivyo, wanatakiwa kufuata sheria, ikiwamo kwenda kwenye Dawati la Jinsia badala ya kuendelea kuvumilia vitendo hivyo ambavyo vina athari nyingi.

Alisema katika mazingira ya aina hiyo, uchumi wa familia unayumba kutokana na mwanamke kuumwa na wakati mwingine kipato cha taifa kinaathiriwa kutokana na mchango wa uzalishaji wa mwanamke kupungua.

"Utafiti wa kitaifa wa Taasisi ya Tanzania Demographic and Health Survey (TDHS) wa mwaka 2010 unaonyesha asilimia 44 ya wanawake wote walioolewa wameshapata ukatili wa kimwili na kingono toka kwa wenzi wao," alisema.

Aliongeza kuwa kwa mujibu wa utafiti huo, asilimia 15 ya wanawake wa Tanzania hawautilii maanani ukatili huo katika ngazi ya familia hali ambayo inasababisha matukio hayo yaendelee kuwapo.

Mmoja wa washiriki wa semina hiyo, Janeth Komba, alikumbusha wanawake kuwa ukatili wa kijinsia ni jambo lolote analofanyiwa mtu kwa hali yake na kumwathiri.

"Anaweza kuathiriwa katika mwili, kiuchumi, kisaikolojia, kingono na hata ukatili wa mtandaoni, hivyo wanawake tusinyamazie vitendo hivyo, badala yake tuchukue hatua zinazostahili ili kukomesha hali hiyo," alisema Janeth.

Mshiriki mwingine, Zahra Omary, alisema Tanzania imeridhia mikataba ya haki za binadamu na kupinga ukatili wa kijinsia.

"Tanzania imetia saini mikataba ya haki za binadamu ili kuondoa aina zote za ukatili dhidi ya wanawake, ikiwamo ya Beijing na Maputo ili kutimiza lengo namba tano la Maendeleo Endelevu," alisema.

Alisema lengo hilo linahusu kuendeleza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake na wasichana, na kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kila binadamu anastahili kuheshimiwa na kupewa hadhi.

HABARI KITAIFA

# Prof. Mwansoko: Nyerere bingwa wa propaganda

**Na Vincent Mpepo,** OUT



MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji (TEKU) Mbeya, Profesa Hermas Mwansoko, amesema Hayati Mwalimu Julius Nyerere ni miongoni mwa magwiji wa propaganda katika siasa za Afrika.

Profesa Mwansoko alitoa kauli hiyo wakati akiwasilisha mada kuhusu 'Mwalimu Julius Nyerere Kama Mwanahistilahi wa Kiswahili' katika Kongamano la Kumbukizi ya Mwalimu Julius Nyerere liliofanyika jijini Mbeya juzi.

Alisema Mwalimu Nyerere alifanikisha utekelezaji wa sera mbalimbali katika harakati mbalimbali za kulitumikia taifa zilizoambatana na propaganda ambazo zilifanikisha kutekelezeka au kutotekelezeka kwa sera kinzani na matakwa ya Watanzania.

"Utekelezaji wa sera ya Azimio la Arusha na nyingine uliambatana na propaganda ambazo zilikuwa na mashiko kwa wakati huo," alisema Profesa Mwansoko.

Alisema utekelezaji wa sera, mipango na harakati mbalimbali ikwamo kupigania uhuru na hata baada ya uhuru propaganda ilihusika na iliendelea kutumika mpaka sasa.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) Mbeya, Dk. Salvatory Mhando, alisema falsafa ya Mwalimu Nyerere kwenye masuala ya kisiasa na uongozi bado ina mashiko kwa kuwa ina uhalisia wa maisha kwa wakati uliopita, uliopo na ujao.

Msomi huyo aligusia wasomi wengi kukimbilia kwenye siasa, akisisitiza kuwa ni suala linalodhoofisha taaluma.

"Wanasiasa wapo tayari kudanganya wananchi ili watimize maslahi yao, kitu ambacho ni hatari kwa ustawi wa nchi kufikia maendeleo ya kweli," alisema.

Mhadhiri na Mkurugenzi wa Kituo cha Mkoa wa Mbeya cha Chuo Kikuu Kikuu Huria cha Tanzania (CKHT), Maulana Ali, aliwataka wananchi kuwa macho na wanasiasa wanaotumia siasa hususani kampeni kama jukwaa kuchafuana na kunyoosheana vidole badala ya kuelezea ilani na mipango ya vyama vyao katika maendeleo ya nchi ikiwa watapewa idhini ya kuongoza.

## Mgombea ubunge CHADEMA aahidi kuboresha kilimo kakao

**Na Thobias Mwanakatwe,** KYELA

MGOMBEA ubunge Jimbo la Kyela kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Alinanuswe Mwalwage, amesema iwapo wananchi watampa ridhaa, atahakikisha anaweka mfumo mzuri kwa wakulima kuuza kakao kwa faida na bila kukopwa.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa kata ya Mababu katika mkutano wa kampeni uliofanyika kijiji cha Kilombero, ikiwa ni mfululizo wa ziara yake ya kuomba kura kwa wananchi.

Mwalwage alisema kakao ambalo ndilo zao kuu la biashara katika Wilaya ya Kyela, bado halijawanufaisha wakulima kuinua maisha yao kutokana na mfumo mbovu wa kilimo na kibiashara.

Alisema mfumo wa ushirika ambao wakulima wanauza mazao yao kwenye mnada si rafiki kwao kwa sababu hawalipwi fedha zao papo hapo na badala yake wanalazimika kusubiri kwa zaidi ya wiki mbili, ili walipwe na kampuni zilizonunua. "Mkinichagua suala la kukopwa kopwa mazao yenu linakwisha. Nitahakikisha mkulima akiuza kakao yake alipwe papo hapo ili kuendesha maisha yake vizuri na kuondokana na umaskini," alisema.

Mwalwage alisema hivi sasa wakulima wanauza zao hilo kati ya Sh. 2,000 na 3,000 kwa kilo wakati bei ingeweza kuwa Sh. 4,000 kama kungekuwa na mfumo mzuri wa ununuzi. Pamoja na kakao, mgombea huyo alisisitiza kuboresha miundombinu ya barabara na kutatua matatizo ya maji na afya ambayo yalikuwa hayajatatuliwa.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaoisaliti Taifa Stars wachukuliwe hatua haraka

**TIMU** ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kuanza kampeni ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2021).

Katika mashindano hayo, Taifa Stars ambayo inafundishwa na Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije, raia wa Burundi, imepangwa kwenye Kundi J ikiwa na Tunisia, Equatorial Guinea na Libya.

Kuelekea katika mashindano hayo, Stars itaanza kibarua chake kwa kuwafuata Tunisia, mchezo utakaochezwa Novemba 13, mwaka huu na baada ya siku nne (Novemba 17, mwaka huu), watarejea nyumbani kuwakaribisha Waarabu hao.

Lakini wakati Stars ambayo mwaka jana ilifuzu kucheza fainali za Afcon baada ya miaka 39, kupita, wiki iliyopita ilikuwa na mchezo wa kirafiki hapa nyumbani dhidi ya majirani zao, Burundi. Mchezo huo wa kirafiki wa kimataifa uliochezwa katika siku inayotambulika kwenye kalenda ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), ulimalizika kwa wageni kuondoka na ushindi wa bao 1-0, shukrani zimwendee mshambuliaji mpya wa Yanga, Saidi Ntibazonkiza, aliyefunga goli hilo pekee.

Jambo la kushangaza lililotokea uwanjani baada ya wageni hao kupata bao, ni kitendo cha mashabiki waliokaa kwenye upande, ambao hutumiwa na wanachama na mashabiki wa Yanga kushangilia goli hilo kwa nguvu, hali ya kuwa wao ni Watanzania. Tukio hilo lilionekana kuwasononesha baadhi ya wadau waliokuwa uwanjani hapo na hata waliokuwa wakiufuatilia mchezo huo kupitia televisheni.

Awali ilionekana kama mashabiki wale walioishangilia Burundi walikuwa mashabiki wao, lakini ilipofuatiliwa, ilibainika walikuwa ni mashabiki wa Yanga na waliendelea kufurahia ushindi huo.

Hakikuwa kitendo cha kiungwana, Taifa Stars inayocheza kwenye ardhi yake na ikitumia uwanja wake wa nyumbani ikizomewa na ikishuhudia wapinzani wao wakipata sapoti. Waswahili wanasema mbuyu ulianza kama mchicha, huu ni wakati mzuri wa wasimamizi wa michezo nchini kuchukua hatua mapema kabla hali haijakuwa mbaya zaidi. Stars inahitaji kupata sapoti na inafahamika wazi kwamba shabiki ni sawa na mchezaji wa 12, je, kama mchezaji huyu wa ziada atahamia kwenye timu pinzani itakuaje? Kitendo cha kumwongezea mpinzani nguvu na kuinyima sapoti Stars si sahihi, ni sawa na makosa mengine ya kuhujumu nchi, wahusika wanatakiwa kuchukuliwa hatua, wasiogopwe.

Awali ilionekana tabia hii ikifanywa na mashabiki wa Simba na Yanga wakati timu zao zinashiriki mashindano ya kimataifa ya ngazi za klabu (Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika), kwa upande mmoja kushangilia timu ya nje, lakini hali hii kuonekana kwenye ngazi ya nchi, inaleta taswira mbaya, haijengi mpira wetu na inaturudisha nyuma.

Nipashe inashauri vyombo husika kuchukua hatua mapema, ili kumaliza 'usaliti' huu, ambao ukiachwa ukaota mizizi, hali inaweza kuwa mbaya zaidi katika siku za usoni.

Kuna taarifa baadhi ya mashabiki wasiokuwa na uzalendo wanaendelea na kampeni 'chafu' ya kujipanga kuwashangilia Tunisia, gazeti hili linaiomba serikali kuweka mikakati ya kuwadhibiti watu hawa kwa faida ya nchi. Kama Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), liliwabaini na kuwafungia mashabiki, ambao walijihusisha na vurugu kwenye mechi za ligi, tunaamini kwa mbinu hizo hizo linaweza kuwachukulia hatua wale wenye nia ya kuisaliti Stars. Tunahitaji kuona Stars inapeperusha vyema bendera ya nchi katika mashindano mbalimbali, ambayo yatasaidia pia kutangaza vipaji vya wachezaji wetu na hatimaye kusajiliwa na klabu za nje ya Tanzania na hivyo kuongeza wigo wa nyota wa kulipwa.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Taifa Stars.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hamna hamna ndimo mliwamo

**MAHALI** panaposemekana hapana kitu huishia kuwa na kitu.

Methali hii hutumiwa hasa pale, ambapo mtu fulani amekuwa akikataa jambo fulani sio kweli, lakini likaishia kuwa alivyokuwa akikataa sivyo.

Leo nawapigania wachezaji wa soka wa hapa Tanzania. Hakika tunao vijana wengi wenye uwezo na akili ya kulichezea 'gozi la ng'ombe, lakini tunashindwa kuwathamini na kuwaendeleza.

Wahenga walisema: "Bura yangu sibadili na rehani (debwani)." Maana yake kitambaa changu duni (bura) sibadili na kingine cha thamani kubwa (rehani). Neno 'rehani' lina maana mbili. Kwa muktadha ninaoujadili, ni kitambaa cha hariri chenye mji wa rangi yoyote na mistari iliyokoza mekundu na kahawia.

Kadhalika "chako ni chako, cha mwenzako si chako." Maana yake kitu unachokiita chako ni kizuri, tena huweza kukufaa na una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine. Tunakumbushwa kuvithamini vitu vyetu. Sizungumzii vitu, bali nazungumzia wachezaji wetu wa kabumbu.

Vilabu vyetu vya kandanda vinaruhusiwa kusajili wachezaji 10 wa kigeni kwa kila timu kwa mujibu wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF).

Kwa mfano, wachezaji wa timu inayoingia uwanjani kucheza ni 11, kwa kila timu duniani kote. Kwa hiyo kama timu moja itasajili wachezaji 10 wa kigeni, na kuchezeshwa wote, ni mchezaji mmoja tu Mtanzania atakayejiunga na wageni 10, ili kukamilisha kikosi kamili kinachotakiwa kuanza mchezo.

Nashindwa kuelewa ni kwa nini au ni sababu zipi muhimu zilizowalazimu (pasa kufanyika jambo, kuwa ni wajibu kufanyika) viongozi wa TFF kuweka kanuni hiyo. Kwamba Tanzania nzima haina wachezaji wanaofaa au? Salala/salale! (tamko linalodhihirisha hisia ya mshangao.) Mbona Tanzania ina wachezaji wengi wazuri kuliko wageni wanaosajiliwa kwa fedha nyingi zaidi ya wenyeji? Fedha nyingi zitumikazo kuwasajili wachezaji wa kigeni na kulipwa mishahara mikubwa zaidi ya wenyeji, kiasi kikubwa hupelekwa nje ya nchi ilhali wenyeji hawalipwi kama walipwavyo wageni!

Yatokeapo mashindano ya kimataifa wakati timu za Ligi Kuu zikiwa kwenye mashindano, wageni waliosajiliwa na timu zetu huitwa kwenda kuzitumikia timu za mataifa yao na kuacha mapengo kwa baadhi ya timu zilizowasajili kwa gharama kubwa.

Kwa sababu hiyo, michezo ya Ligi Kuu husimamishwa, ili kuzipa ahueni/afueni timu zilizochukuliwa wachezaji wao. Mara nyingi timu zenye wachezaji wengi wa kigeni ni Azam, Simba na Yanga.

Kwa sababu hiyo, ligi husimamishwa, ili kuzipa nafasi timu hizo 'kuu' kuwasubiri wachezaji wao wa kigeni waliotwa makwao! Nawakumbuka wahenga wetu waliosema "Cha kupewa hakishibishi." Maana yake kitu cha kupewa hakiwezi kumshibisha mtu.

Ligi Kuu inaposimamishwa kwa sababu ya timu tatu tu zitwazo 'kubwa' kuondokewa na wachezaji wao watatu wanaokwenda kuziwakilisha nchi zao kwenye michuano ya kimataifa, husababisha ligi kuvurugwa na kusimamishwa kwa muda.

Kwa sababu hiyo, ratiba ya Ligi Kuu hubadilishwa. Kwa hali hiyo, timu zisizo na wachezaji wa kigeni hupangiwa mechi za kucheza. Hivyo Azam, Simba na Yanga huwa na fursa ya kufanya mazoezi zaidi wakati wachezaji wao wa kigeni waliokwenda makwao kushiriki michezo ya kimataifa wakisubiriwa kwa udi na uvumba ndipo waanze na ratiba iliyobadilishwa!

Kwa mtazamo wangu, TFF ambayo baadhi ya wachora katuni wanaiita 'Tifua Tifua' inapaswa kufikiri upya kuhusu ruhusa ya timu zetu kusajili wachezaji 10 wa kigeni.

'Kufikiri upya' nina maana ya kuanzisha shule za kuwafundisha vijana mchezo wa kandanda unaopendwa zaidi duniani. Tutakapokuwa na wachezaji watakaosajiliwa nje ya nchi, Tanzania itaingiza fedha za kigeni, badala ya kuzinufaisha nchi hizo kwa fedha zetu adimu (-enye kupatikana kwa uchache au shida) za kigeni. Fikiri kama kila mkoa wa Tanzania itakuwa na shule yake ya kuwafundisha vijana mchezo wa mpira, nchi ingekuwa na shauku (hamu kubwa ya kutaka kufanya jambo) ya kusajili wachezaji wa kigeni?

Kadhalika kama tungekuwa na utaratibu wa kuwapeleka walimu wa kandanda kujifunza katika nchi kama Brazil, Hispania, Italia, Ujerumani, Ufaransa n.k. leo Tanzania ingekuwa na walimu wazuri wa kandanda wanaofundisha timu mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Vilevile kusingekuwa na sababu ya kutumia fedha zetu adimu za kigeni kuwaajiri Wazungu wanaohitaji fedha nyingi na kutunzwa vizuri kuliko walimu wetu wananchi wasiothaminiwa wala kuheshimiwa na walimu Wazungu!

Baadhi yao huonyesha wazi ubaguzi wa rangi. Ebo! (tamko linaloonyesha hisia ya dharau inayotokana na kukasirika au kutoridhika). Fedha tunawapa sisi lakini wanawadharau walimu wetu ambao ndiwo wenye nchi yao? Abadan! (tamko la kukataa au kukanusha uwezekano wa kutokea jambo).

# Shule yakabiliwa na uhaba matundu choo

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

Shule ya msingi Ibinzamata iliyoKo Manispaa ya Shinyanga, inakabiliwa na upugufu wa matundu 32 ya choo, hali ambayo imedaiwa kuhatarisha afya za wanafunzi sababu ya kukosa mazingira bora ya kujisaidia.

Mwalimu wa Afya katika shule hiyo, Mkami Matutu, alibainisha hayo juzi wakati maofisa afya wa manispaa ya Shinyanga, walipokuwa wakitoa elimu ya unawaji mikono kwa wanafunzi, kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV).

Alisema shule hiyo ina wanafunzi 1,065 wavulana wakiwa 483 na wasichana 582, huku mahitaji ya matundu ya vyoo yakiwa 48 lakini yaliyopo ni 16 tu, hivyo kuwa na upungufu wa matundu 31.

Kutokana na upungufu huo, Mwalimu Matutu alisema hali hiyo inahatarisha afya za wanafunzi na walimu.

"Tunashukuru sana maofisa afya kufika hapa shuleni kwetu na kutoa elimu ya unawaji mikono kwa wanafunzi pamoja na kutupatia kifaa cha kisasa cha kunawia mikono. Lakini tuna kabiliwa na changamoto kubwa ya upungufu wa matundu ya choo 32," alisema Matutu.

Naye Mkuu wa Idara ya Mifugo Manispaa ya Shinyanga, Mohamed Chanzimu, akimwakilisha Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Geofrey Mwangulumbi, alisema changamoto hiyo ameisikia na ataiwasilisha kwa mkuu wake ili shule hiyo itengewe bajeti ya ujenzi wa matundu ya choo.

Aidha, Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira Manispaa ya Shinyanga, Kuchibanda Snatus, akitoa elimu kwa wanafunzi hao, aliwataka wazingatie suala la unawaji mikono mara kwa mara, hasa pale wanapotoka kujisaidia chooni, ili kuimarisha usafi na kukabiliana na magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu.

Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Ibinzamata, akiwamo Amina Sayi, walishukuru kupewa elimu hiyo pamoja na kifaa cha kisasa cha kunawa mikono na kuahidi kukitumia vizuri ili kujilinda na magonjwa ya mlipuko yatokanayo na uchafu ama kula kinyesi.

# Majaliwa asema JPM ndiye chagua sahihi

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, amewaomba Watanzania wote wakiwamo na wakazi wa wilaya ya Karatu wajitokeze kwa wingi kwenda kumchagua Rais John Magufuli ambaye ni mgombea urais wa CCM.

Majaliwa amesema wananchi wanapaswa kumchagua kiongozi huyo kwa sababu ni kiongozi sahihi.

Majaliwa alisema hayo jana alipozungumza na wakazi wa Karatu kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika katika uwanja wa Mazingira Bora wakati akimwombea kura Rais Magufuli pamoja na mgombea ubunge wa Jimbo la Karatu, Daniel Awack na wagombea udiwani wa CCM.

"Dk. Magufuli ni kiongozi sahihi atakayeweza kuratibu maliasili zetu na kuzikusanya pamoja kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. Mnajua tulivyokuwa tunaibiwa katika madini lakini leo hakuna anayetuibia ni kwa sababu ya kuwa na kiongozi mwadilifu anayeweza kuongoza na kuwatumikia wananchi wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

"CCM ndicho chama pekee kitakachowaletea maendeleo na hamtojuta kuwachagua viongozi wa CCM. Mambo yote ya maendeleo Karatu yamo ndani ya Ilani. Kitabu cha Ilani kimejaa miongozo na maelekezo ya kuwatelea maendeleo Watanzania wote. Tumpe Dk. Magufuli ridhaa ya kuongoza miaka mitano mingine ili atuletee maendeleo," alisema.

Amesema wananchi wanatakiwa wamchague Dk. Magufuli ili aendelee kuwaletea maendeleo kwa sababu katika kipindi cha miaka mitano ya awali amefanya mabadiliko makubwa katika huduma mbalimbali za jamii zikiwamo afya, elimu, maji na miundombinu.

Kuhusu usambazaji wa umeme, Majaliwa alisema zaidi ya vijiji 9,300 nchini vimefikishiwa nishati hiyo kutoka vijiji 2,018 mwaka 2015, hivyo hali ya upatikanaji wa umeme imeimarika, watumiaji wa umeme wameongezeka kutoka asilimia 35 hadi 85 hivi sasa.

Aliwahakikishia wananchi hao kwamba vijiji vyote 10 vya wilaya hiyo ambavyo bado havijafikiwa na nishati ya umeme vitafikiwa. Wilaya ya Kataru ina vijiji 57 kati yake vijiji 47 tayari vimeshaunganishiwa umeme.

Majaliwa alisema Rais Magufuli anataka kuona kila nyumba ya Mtanzania inapata umeme tena kwa gharama nafuu na ametenga fedha nyingi zitakazotosheleza kusambaza umeme katika vijiji vyote vikiwamo na wilaya ya Karatu. Gharama za kuunganishiwa umeme huo amezipunguza kutoka Sh. 177,000 hadi Sh. 27,000 tu.

Pia alisema wananchi hawatowajibika tena kulipia gharama za nguzo wala hawatalipia fomu za maombi ya kuunganishiwa huduma hiyo kwa sababu tayari gharama hizo zote zimebebwa na serikali.



Mshauri wa ubunifu wa majengo na ukadiriaji majenzi, Dk. Stanslaus Ntiyakunze, akitoa mada jijini Dar es Salaam jana, kwa wahandisi kuhusu kufuata utaratibu wa mikataba, kwenye mkutano wa mwaka wa Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yajizatiti kuwaondolea wanawake vikwazo vya kiuchumi

**Na Julieth Mkireri,**
MKURANGA

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara ya Maendeleo ya Jamii), Dk. John Jingu, amesema serikali inaendelea kufanya jitihada za kuondoa vikwazo kwa mwanamke anayeishi kijijini ili kumwezesha kutoa mchango katika uzalishaji kiuchumi.

Dk. Jingu alibainisha hayo jana katika maadhimisho ya Siku ya Mwanamke Anayeishi Kijijini na uzinduzi wa kampeni ya Nyumba Bora iliyofanyika katika Kijiji cha Kazole, Mkuranga mkoani Pwani.

Alisema, serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuhakikisha mwanamke wa kijijini anakuwa na uwezo wa kiuchumi kwa kuanzisha mifuko ya mikopo na kuhamasisha uundaji wa vikundi ili wakopesheke kwenye halmashauri na taasisi mbalimbali.

"Mwanamke wa kijijini ni msingi wa maendeleo ya kijamii kwa kuwa wao ndiye mlezi na msingi wa uzalishaji. Serikali inamthamini mwanamke wa kijijini na itaendelea kuboresha mazingira yake kiuchumi," alisema.

Dk. Jingu aliwapongeza maofisa maendeleo ya jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga kwa kuchochea maendeleo kwa wananchi na kusisitiza kuachana na tabia ya kukaa ofisini.

Aidha, alikipongeza kikundi cha wanawake cha Upendo kwa kuonyesha mfano wa kuwa na kikundi cha VICOBA ambacho kimeanza kuonyesha mfano wa kuboresha makazi yao

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Pwani, Grace Tete, alisema mkoa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, wanaboresha makazi kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini na kwamba elimu inatolewa kwa wananchi.

Tete alisema ili kukabiliana na vikwazo hivyo, mkoa unahamasisha uanzishwaji wa vikundi vya kuweka na kukopa vitakavyowawezesha mwananchi wa kipato cha chini kuweka na kukopa na kupata fedha za masharti nafuu zitakazoboresha makazi yao.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Mkuranga, Veronica Kinyemi, alisema kupitia vikundi vya VIKOBA, wananchi wa wilaya wameanza kuboresha makazi yao. Alisema kwamba katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 Sh. milioni 700 zimetengwa kwa ajili ya kukopesha vikundi vya ujasiriamali vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

# TAKUKURU yaokoa nyumba

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Pwani, imerejesha nyumba ya Mayasa Mmeleke iliyokuwa ikishikiliwa na kutaka kuuzwa na Godlisten Ndimbo kwa deni la Sh. milioni 1.8.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Suzana Raymond, alisema jana kuwa Mayasa alikopa Sh. milioni tatu kutoka kwa Ndimbo kwa makubaliano ya kulipa riba ya Sh. milioni 1.2 na kuweka rehani hati ya nyumba.

Alisema mkopaji aliweka rehani hati yake ya nyumba namba MZR/MKZ/641 iliyoko Kitongoji cha Mkuza wilayani Kibaha na hadi Novemba mwaka jana, alikuwa amerejesha Sh. milioni 2.4 kati ya Sh. milioni 4.2 alizopaswa kulipa.

"Kiasi kilichokuwa kimebaki ndiyo kilipelekea mkopeshaji kutaka kuuza nyumba ya Mayasa, kitu ambacho ni dhuluma. TAKUKURU ilifanya uchunguzi wa kina na kubaini ukiukwaji mkubwa wa sheria uliofanywa na mkopeshaji kwa kufanya biashara ya ukopeshaji wa fedha bila kusajiliwa, kinyume kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Benki yaani 'Banking and Financial Act' ya Mwaka 2006," alisema Suzana.

Alisema kifungu hicho kinakataza mtu kufanya shughuli za kibenki au kutoza riba pasi na leseni kutoka Benki Kuu (BoT) na mkopeshaji alibainika kukwepa kulipa kodi kutokana na biashara hiyo anayoifanya kinyume cha Sheria. Akizungumzia kazi walizofanya kwa kupindi cha miezi mitatu kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu, kiongozi huyo wa TAKUKURU alisema ofisi yake ilipokea malalamiko 318 na kati yake, 157 uchunguzi wake unaendelea katika hatua mbalimbali na malalamiko 74 yalionekana kuangukia katika sheria nyinginezo, hivyo walalamikaji walishauriwa na kuelekezwa sehemu husika kwa lengo la kutatua kero zao.

Alisema kesi 34 ziliendelea kuendeshwa katika mahakama mbalimbali za Mkoa wa Pwani na kesi 10 zilitolewa hukumu na Upande wa Jamhuri ulishinda kesi sita kwa washtakiwa kuhukumiwa kifungo jela au kulipa faini na kesi nne watuhumiwa hawakukutwa na hatia, hivyo waliachiwa huru.

"Katika kushughulikia malalamiko yaliyowasilishwa, ofisi imefanikiwa kuokoa mali mbalimbali zikiwamo fedha Sh. milioni 6.4 kwenye akaunti ya Halmashauri ya Chalinze," alibainisha.

Suzana pia alisema waliokoa viwanja vya watumishi 12 waliokuwa wanadai mishahara kwa kazi ya ulinzi katika Kampuni ya PRC Associates Security (T) Ltd ya mjini Kibaha.

Alisema watumishi hao walifanya kazi katika kampuni hiyo ya ulinzi kwa takribani miaka mitatu pasi na kulipwa mishahara yao na kufanya jumla ya deni la mishahara wanayodai kufika Sh. milioni 23.

# Kishimba aibuka na mbinu mpya kampeni

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MGOMBEA ubunge wa Kahama Mjini, Jumanne Kishimba (CCM), ameibuka na staili mpya ya kuomba kura kwa wananchi kwa kuweka ujumbe wa sauti akichangia mijadala bungeni.

Katika michango yake hiyo anayoitumia kushawishi wananchi kumpigia kura Oktoba 28 mwaka huu, umo unaohusu kukipigia debe kilimo cha bangi na biashara ya pombe kali ya kienyeji aina ya gongo.

Kishimba aliweka ujumbe huo jana wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Nyahanga, Halmashauri ya Mji wa Kahama katika mkutano wa hadhara kwa ajili ya kampeni.

Mgombea huyo amekuwa akiweka ujumbe huo na kuwasikilizisha wananchi kabla ya kuomba kura. Aliwaomba wananchi kuchagua viongozi ambao watakuwa na hoja mpya na zenye mashiko ili kuwaletea maendeleo.

Alisema kuwa yeye alishawishi serikali na kujenga masoko ya madini nchi nzima, jambo ambalo kwa sasa limesaidia serikali kutoibiwa tena dhahabu na kufuta tozo mbalimbali.

Hata hivyo, baadhi ya wananchi wa jimbo hilo walimtaka Kishimba kuacha kutumia muda mwingi kuweka sauti za aliyozungumza akiwa bungeni badala yake ajikite kwenye kuuza ilani ya chama.




Mgombea ubunge wa Jimbo la Rufiji, mkoani Pwani, kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mohamedi Mchengerwa, akihutubia mkutano wa kampeni katika kijiji cha Nchumbi, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ahamasisha unywaji maziwa, ulaji nyama

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewataka Watanzania kujenga utamaduni wa kunywa maziwa yaliyosindikwa na bidhaa zake pamoja na kula nyama bora zilizozalishwa, kuchakatwa na kukaguliwa na wataalamu wa mifugo.

Katibu Mkuu wa Mifugo katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, alitoa wito huo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika Njombe.

"Tujizoeshe na watoto wetu kutumia bidhaa za mazao ya mifugo zilizosindikwa na kuchakatwa ikiwa pamoja na maziwa freshi, mgando, jibini, samli, siagi, na hata maziwa ya unga.

"Bidhaa zote hizi ni bora, salama, zinajenga afya bora na kuongeza kiwango cha ufahamu kwa watoto," alisema.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo, kiongozi huyo alisema hadi mwezi uliopita jumla ya shule 210 zenye wanafunzi 89,922 zimenufaika na mradi wa maziwa shuleni katika mikoa 10.

Aliitaja mikoa iliyonufaika kuwa ni Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Njombe, Morogoro, Mwanza na Mara.

Alisema lita 12,023,186.83 za maziwa zenye thamani ya takribani Sh. bilioni 19.24 zimenywewa katika vipindi tofauti kuanzia mwaka 2006 hadi 2020. "Kwa mwaka 2020/21 programu za unywaji maziwa zinaendelea kutekelezwa katika shule 30 kutoka shule 210 zilizokuwa zikitekeleza mapango huo hapo awali. Mikoa inayotekeleza mpango huu kwa sasa ni Kilimanjaro (Shule 24), Iringa (Shule 2) na Mbeya (Shule 4) na hii ni kwa ushirikiano wa wazazi na wasindikaji," alisema. Alisema kufanyika kwa maadhimisho hayo mkoani humo imekuwa ni chachu ya kuwashawishi wadau wa maziwa, viongozi wa serikali, wa kisiasa na kidini kushirikiana na wazazi kuhakikisha mpango huo unatekelezwa katika shule zote.

"Wizara imejipanga kuhakikisha uzalishaji wa maziwa unaongezeka ikiwa ni pamoja na kuongeza ushirikiano na wadau wa tasnia ya maziwa," alisema.

Prof. Gabriel alisema kutoka mwaka 2015/16 hadi mwaka 2019/20 Tanzania imefanikiwa kuwa na jumla ya viwanda vipya 17 vya kusindika nyama na kufanya kuwa na jumla ya viwanda 99 nchini vya kuchakata maziwa, vyakula vya mifugo na nyama.

Alisema wastani wa kusindika maziwa umeongezeka kutoka lita 167,520 mwaka 2015/2016 hadi lita 203,600 kwa siku katika mwaka 2019/2020.

Prof. Gabriel alisema sekta ya uvuvi inachangia asilimia 30 ya protini inayopatikana na wanyama na inatoa ajira kwa Watanzania takribani milioni 4.5 katika shughuli zinazohusiana na uvuvi. Alisema Tanzania ni nchi ya pili Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo ikiwa na ng'ombe milioni 33.4, mbuzi milioni 21.29, kondoo milioni 5.65, kuku milioni 83.28, nguruwe milioni 2.14 na punda 657,389.

Alisema ng'ombe hao katika mwaka wa 2019/20, wameweza kuzalisha lita bilioni 3.01 ambapo lita bilioni 2.1 zimetokana na ng'ombe wa asili na lita bilioni 0.9 zimetokana na ng'ombe wa kisasa. Alisema tani 701,679.1 za nyama ziliweza kuzalishwa katika kipindi cha mwaka 2019/20 ikilinganishwa na tani 690,629 zilizozalishwa mwaka 2018/19.



## HABARI DODOMA

# Wafanyabiashara watakiwa kuacha kuwa mtaji wa siasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wadogo wametakiwa kuacha kutumika kama mtaji wa wanasiasa kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara hao Wilaya ya Dodoma, Baraka Mrisho, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya uchaguzi huo, jijini hapa. Mrisho alisema ni wakati wa wafanyabiashara hao kuwa makini katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu kwa kuwa wanasiasa wengi wamekuwa na maneno matamu ya kuvutia ambayo yanaweza kusababisha wakajikuta wanafanya makosa ya kutumika kisiasa.

"Tuepukane na wanasiasa ambao wanataka kutufanya sisi kama mtaji wao wa kisiasa ili kuwanufaisha wao na maslahi yao binafsi si taifa," alisema Mrisho.

Pia aliwaomba kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura ili kumchagua kiongozi bora atakayeendeleza mazuri yaliyofanyika katika miaka mitano iliyopita.

"Sisi kama wamachinga hivi sasa tunafanya biashara zetu bila kubugudhiwa kama ilivyokuwa hapo zamani kukimbizwa na migambo wa jiji, lakini serikali imetusaidia kwa kutupatia vitambulisho ambavyo vinatusaidia kufanya biashara kwa amani," alisema Mrisho.

Pia alisema kuwa itakuwa jambo la busara kama wajasiriamali watajitokeza kwa wingi ili kumchagua Rais John Magufuli, kuendelea kuboresha katika maeneo yale ambayo aliyaanza kuyafanya katika muhula wake wa kwanza. "Niwaombe wajasiriamali wote nchini tuondoe itikadi za vyama vyetu na tuionyeshe dunia kuwa serikali yetu hii chini ya Rais Magufuli ni ya kizalendo kwa kuichagua kwa kura nyingi za kishindo ambazo hazijawahi kutokea hapo awali," alisema.

Kadhalika, aliwataka wajasiriamali wote kufanya shughuli zao za biashara kwa kuzingatia taratibu na sheria zilizowekwa na halmashauri zao za miji na majiji.

"Wajasiriamali wakati mwingine tunavunja sheria za nchi kwa kujiona kuwa sisi ndio wenye haki kuliko watu wengine unakuta muda mwingine tunapanga bidhaa zetu hadi katika maeneo ya barabara hadi magari yanashindwa kupita," alieleza Mrisho.



Kontena la kuhifadhia takataka likiwa limejaa na zingine kutapakaa chini karibu na makazi ya watu eneo la Chang'ombe, jijini Dodoma jana, kitendo ambacho ni hatari kwa afya za wakazi wa eneo hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kanisa laomba jamii kuwajali walemavu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KANISA la The Free Pentecostal Tanzania (FPCT) limeomba jamii inayoishi na watoto wenye ulemavu kuwaendeleza kielimu hadi kufikia chuo kikuu badala ya kuwaacha majumbani.

Mratibu Mkuu wa Mradi wa Elimu Jumuishi kutoka kanisa hilo, Lucas Mhenga, alitoa ombi hilo alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha pamoja kilichowajumuisha wafanyakazi wa jiji, wazazi na walezi kwa ajili ya uanzishaji wa Baraza la Watoto Wenye Ulemavu Wilaya ya Dodoma.

Alisema jamii inatakiwa kuwasomesha watoto hao kuanzia ngazi ya chini hadi chuo kikuu badala ya kuendelea kuwaweka majumbani, huku wakiteseka kwa kukosa haki hiyo ya msingi ya kupata elimu.

"Bado kuna ukatili, ubaguzi na manyanyaso kwa watoto wenye ulemavu majumbani (kwenye makazi). Walio wengi wamekosa elimu, matibabu na hata haki zao za kimsingi kama wanadamu wenzao," alisema.

Akizungumza kuhusu uanzishaji wa baraza hilo, alisema limelenga kuwatambua watoto wenye ulemavu na kuwakutanisha ili wawe na sauti moja itakayowafanya kuzijua haki zao za msingi na wajibu.

Kadhalika, alisema lengo lingine ni kuwajengea uwezo mabaraza mengine ya watoto ulemavu katika kila ngazi husika ili kujumuika pamoja.

"Baraza la Watoto limekusudia kupiga vita aina zote za imani potofu zinazosababisha kuwatendea ukatili watoto wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na mauaji yanayoendelea ya kuwakata viungo vyao," alisema.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Vijana Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalang'anya, aliwataka wazazi wenye watoto ambao wana ulemavu kutowaona kama ni sehemu ya mkosi kwenye familia.

# EWURA sasa yaja kidijitali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji(EWURA), imeanzisha mfumo wa kitaifa wa kidijitali wa ukusanyaji, uratibu na uunganishaji wa taarifa za sekta ya petroli na gesi asilia (NPGIS).

Akizungumza jana kuhusu mfumo huo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, alisema mfumo huo utawezesha upatikanaji wa taarifa za kila siku, wiki na mwezi na kutoa ripoti anuwai za masuala hayo nchini.

"Mfumo utaihudumia EWURA, Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na taasisi zote za serikali za kimkakati," alisema.

Mhandisi Chibulunje alisema NPGIS ni kitovu cha kukusanya na kuchangamanisha taarifa kwa pamoja za masuala ya petroli na gesi asilia nchini, ili kupata takwimu sahihi kwa utekelezaji na ufanisi wa shughuli za kiudhibiti na ukusanyaji mapato ya serikali.


Alitoa wito kwa wadau wote kushirikiana katika kuhakikisha mfumo huo unakuwa na tija kwa kuwasilisha taarifa husika kwa wakati.

"Huu mfumo utaunganishwa na mifumo mingine ya serikali hivyo taasisi zinatakiwa kuwasilisha taarifa husika kwa wakati, kwa kuwa si tu utainufaisha EWURA bali wadau wote wa sekta ya mafuta na gesi asilia nchini," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Petroli wa EWURA, Gerald Maganga, alisema kupitia mfumo huo, EWURA itapata kwa urahisi taarifa za makisio ya mahitaji ya mafuta, uingizaji wa mafuta kwa aina nyingi.

Pia alisema bei na chanzo, taarifa za kutolewa kwa mafuta melini kwenda ghalani, ikiwa ni pamoja na jina la chombo, aina ya bidhaa na muda wa kutoka.

"Huu mfumo utasaidia kutambua akiba ya mafuta kwa aina na wingi katika miliki ya wauzaji, mauzo na matumizi pamoja na mambo mengine," alisema.





# Ataka jitihada za wadau wote kukabili maafa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, Makame Khatib Makame, amesema nguvu za pamoja zinatakiwa ikiwamo ushirikishaji wa wadau katika kupambana na majanga.

Akizungumza jana katika kikao cha kujadili mwongozo wa kukabiliana na maafa Zanzibar huko Maruhubi, alisema endapo wadau wataunganisha nguvu katika mipango na mikakati kupitia sera ya maafa, watasaidia kupunguza athari za maafa nchini. Alisema mwongozo huo utawasaidia watu wenye mahitaji maalum, watoto na watu wazima kupata elimu ya kukabiliana na maafa ili kujikinga, kukabiliana na kurejesha hali baada ya maafa kutokea.

Makame aliwataka masheha na kamati za maafa kuendeleza na kusimamia mikakati ya kutoa elimu ili kuiwezesha jamii kupata uwelewa wa kujihami na kujilinda maafa yanapotokea.

Naye Mshauri Mwelekezi wa Mwongozo huo kutoka Maahad Istiqama Tunguu, Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (Suza), Mussa Juma Mzee, alisema jamii ifahamu njia bora ya kukabiliana na maafa na majanga ya kimaumbile na ya kusababishwa na binadamu.

Alibainisha kuwa mwongozo huo utatoa mbinu za ufundishaji na kujua jinsi ya ufahamu kwa walioфundishwa .

"Lengo la mwongozo huu ni kuwa na utaratibu ambao utawasaidia mfundishaji na mfundishwaji kwenda sambamba katika kufahamiana ili kufikia malengo yaliyokusudiwa," alisema.

# UVCCM: Mwinyi anakubalika Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Zanzibar (UVCCM), umesema umefanya tathmini ya mikutano ya kampeni za mgombea wa urais wa chama hicho Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, na kubaini kuwa anakubalika na wananchi.

Kukubalika huko ni baada ya kufanikiwa kuyafikia makundi 52 ya kijamii ya watu mbalimbali Unguja na Pemba tangu alipozindua kampeni zake mwezi uliopita.

Naibu Katibu Mkuu wa UVCCM, Mussa Haji Mussa, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa na kusema hakuna mgombea wa urais aliyefanikiwa kuyafikia makundi hayo muhimu hadi sasa.

Aliyataja makundi yaliyofikiwa hadi sasa ni vijana wa aina mbalimbali wakiwamo wasomi wa vyuo vikuu vya Zanzibar, wajane, wakulima wa mazao ya kilimo na mwani, wavuvi na wajasiriamali, mamalishe na waendesha pikipiki, maarufu kama bodaboda.

Mussa alisema kitendo cha kuyafikia makundi hayo kwa kufuata katika sehemu wanazofanya shughuli zao ikiwamo vijijini, zinadhihirisha nia na malengo ya mgombea huyo kwamba akishinda yuko tayari kuzipatia ufumbuzi changamoto zote zinazowakabili.

"UVCCM imefanya tathmini ya kampeni za mgombea wa urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM na kuridhishwa nazo kwa sababu ni mgombea pekee aliyefanikiwa kuyafikia makundi yote muhimu ya kijamii Unguja na Pemba," alisema.

Alisema sera ya uchumi wa buluu ni mategemeo makubwa ambayo yanaweza kuzalisha ajira nyingi kwa vijana wavuvi kuyafikia maeneo ya bahari kuu na kuacha kuvua maeneo yenye kina kidogo ambayo mara nyingi husababisha migogoro. Hadi sasa, alisema eneo la bahari kuu halijatumiwa kikamilifu na wavuvi wazawa kwa kuvuna rasilimali zilizopo, hivyo kuwachukua wavuvi wengine zikiwamo meli za kimataifa zilizosajiliwa kuvua maeneo hayo na kuingiza kipato kikubwa.

"Umoja wa Vijana wa (CCM) umejenga matumaini makubwa kwa Dk. Mwinyi ambaye ameahidi ajira 300,000 katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ambazo hizo kati yake zitatoka katika uchumi wa bluu kwa kuyafikia maeneo ya bahari kuu," alisema.

Pia alilitaja eneo lingine ambalo bado halijatumiwa vizuri na vijana kuwa ni sekta ya kilimo cha aina mbalimbali kama vile mboga na viungo, ambalo ni chanzo kimojawpo cha ajira.

Mussa alisema sekta ya kilimo ina nafasi kubwa katika kuzalisha ajira kwa vijana huku likiwapo eneo kubwa la ardhi kwa ajili ya kuzalisha bidhaa mbalimbali za chakula. Alisema Umoja wa Vijana umefurahishwa na kazi kubwa iliyofanywa na mgombea huyo alipowatembelea wakulima wa mwani, zao ambalo hulimwa kwa asilimia 90 na wanawake.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa ukuta wa uzio wa kituo kipya cha mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani kilichopo Mbezi Luis, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Taasisi elimu yawaangukia walimu uboreshaji mitaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TAASISI ya Elimu Zanzibar imewataka walimu wakuu wa shule mbalimbali kuichangia vizuri kanuni ya sheria ya taasisi hiyo ili kuimarisha ubora wa elimu nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo, katika kikao cha kuimarisha kanuni kilichofanyika jana mjini hapa, Kaimu Meneja wa Mitaala na Vifaa wa Taasisi hiyo, Abdalla Mohammed Mussa, alisema ili kanuni zikae kwa muda mrefu, ni lazima zipate maoni madhubuti ambayo yatalenga kuimarisha elimu.

Kaimu meneja huyo alisema Taasisi ya Elimu Zanzibar ina wajibu wa kupitia mitaala ya elimu kwa ngazi zote kuanzia maandalizi hadi sekondari ikishirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE) ambao wao ndio wahusika wakuu wa mitaala ya elimu ya sekondari.

Alisema taasisi hiyo pia ina jukumu la kupitia mitaala ya vyuo vya ualimu vya Zanzibar ambavyo ndivyo vinavyotoa walimu ambao wanafundisha katika shule za Zanzibar na hata nje ya Zanzibar.

Pia alisema taasisi ina jukumu la kufanya utafiti wa kielimu ili kushajihisha mapitio ya mtaala na kupitia vitabu.

Naye Mwanasheria kutoka Taasisi ya Elimu Zanzibar, Kondo Malik Kondo, alisema kuwa kanuni hizo ni miongozo ya kuimarisha elimu ya Zanzibar na kuna malalamiko mengi juu ya ukuaji wa elimu pamoja na njia za utoaji wa elimu kwa walimu wa shule mbalimbali.

Baadhi ya washiriki wa kikao hicho waliitaka taasisi hiyo kuangalia upya mitaala ya elimu ya maandalizi kwa kuzingatia wingi wa masomo kwa wanafunzi na wanatakiwa zaidi wajue kusoma, kuandika na kuhesabu na sio kupatia masomo mengi ambayo itakuwa ni mzigo kwao. Pia waliishauri taasisi hiyo kuangalia sheria ya uuzaji wa vitabu vya serikali kwa kuwawajibisha wauzaji na hata wanunuzi kwani nao pia ni wakosa kisheria.

Kikao hicho kiliwashirikisha walimu wakuu wa shule za serikali na za binafsi za Unguja.






Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE







VITA JUKWAANI

# Diamond, Kiba, Harmonize liwe jua...

WAKATI kampeni za kuhitimisha uchaguzi mkuu zikiendelea, wasanii wa muziki wa Bongo Fleva, wamekuwa wanufaika wakubwa baada ya vyama vya siasa kuwatumia katika ushawishi wao kwa wapigakura.

Wanamuziki mbalimbali wamekuwa wakipanda jukwaani kutoa burudani wakati vyama hivyo vikiwanadi wagombea wao, kutokana na ukweli kwamba sanaa ina nguvu ya kusikilizwa na watu.

Baadhi ya wasanii waliokuwa katika kampeni hizo ni Diamond Platnumz, Ali Kiba, Harmonize, Zuchu, Chege na wengine wengi.

Hata hivyo, kivutio kikubwa ni vita vya jukwaani vinavyoendelea kati ya vinara wa muziki huo, Diamond, Ali Kiba na Harmonize, ambao licha ya kutoa burudani tosha kwa wanachama wa vyama hivyo, pia wameongeza joto kwa mashabiki wao.

Wasanii hao kila mmoja anatumia mbinu mbalimbali katika kuwashawishi watu kumwona bora zaidi ya wengine, jambo ambalo limezidisha ubunifu katika shoo zao.

Diamond Platnumz, anaonekana kuwashinda wenzake kwa uburudishaji wake uliojaa ubunifu na vionjo ambavyo vinawaacha watu wakiwehuka kwa furaha.

Baadhi ya ubunifu ni kuimba na kucheza na mashabiki wake, kuwatumia wanenguaji mahiri na kucheza miondoko ya Michael Jackson, ambayo umnogesha zaidi.

Ali Kiba, naye hajaachwa nyuma katika vita hiyo, kwani licha ya kutumia maneno ya vijembe, amekuwa tofauti zaidi baada ya kuanza kuwatumia wanenguaji katika shoo zake za jukwaani.

Harmonize, ambaye anajiita 'Jeshi' yeye anatumia mbinu za medani kama njia ya kuwavutia mashabiki na kuonekana tofauti. Mara nyingi akipanda jukwaani anavaa magwanda na kubeba begi mgongoni ili kuonekana ni mkakamavu zaidi ana anayeweza kupambana.

Akipanda jukwaani, Harmonize hawatumii sana wanenguaji, badala yake yeye mwenyewe anakuwa burudisho tosha kwa mashabiki wake.

BASI SAWA

## Hanstone pole yaliyokukuta

MSANII wa Bongo Fleva, Hanstone, amesimulia jinsi watu waliovamia studio za mtayarishaji wa muziki S2Kizzy, akisema yeye miongoni mwa watu waliopigwa na kujeruhiwa.

Hanstone amesema amepigwa na watu hao ambao walijitambulisha kuwa polisi jamii, kisha kuporwa mali zao ikiwamo simu za mikononi.

"Mimi ni mmoja wapo kati ya niliyevamiwa na watu waliokuwa wakidai ni polisi jamii studio kwa S2Kizzy na kupigwa bila hatia, kuumizwa na kuibiwa," amesema Hanstone.



## Official Nai atakagi wivu

MPAMBAJI wa video za muziki, Official Nai, ametaja chanzo cha kuachana na mpenzi wake, Moni Centrozone, kuwa wivu na hisia za kusalitiwa.

Official Nai, amesema Moni Centrozone, alikuwa anahisi yeye ana uhusiano na mfanyabiashara wa mavazi tangu kipindi cha nyuma, kabla ya kutamka hadharani siku za hivi karibuni.

"Sijawahi kutoka na Fred japo ikitokea naweza kuwa naye ila kwa sasa sijawaza na sijafikiria, kwanza mimi na yeye tumeongea mara moja tu tangu suala hili kuanza kuzungumziwa zaidi mitandaoni anaona kama nimefanya kiki, Moni alianza kuhisi hivyo muda mrefu na tumeachana mwezi wa tatu au wanne, yeye ndiyo aliumiza sana moyo wangu " amesema Official Nai.





## Uchebe amzulia jambo Masha Lovie

MWANAMITINDO na mkufunzi wa wapambaji wa video za muziki, Masha Lovie, amepinga kuwa yeye anamkuwadia Uchebe kwa wanawake wengine.

Masha Lovie 'Don Dada', ameamua kutoa kauli hiyo baada ya kuonekana akiwa karibu na mpenzi wa Uchebe aitwaye Agness, hivyo kusababisha watu waamini yeye amekuwa mtu wa kati katika penzi hilo.

"Uchebe ni mshkaji wangu tangu yupo na Shilole, kwanini wanasema kwamba nimempa mwanamke, mahusiano yake mapya na mtu wake hata hayanihusu, nilivyonunua gari mtu wa kwanza kumwita ni Uchebe ili kuliangalia na kunisaidi kwenye mambo ya usajili, TRA na bima," ameongeza.

# Mfuko Mweusi: Siri inapopenya mitaani

**Na Adam Fungamwango**

MARA nyingi binadamu hupata matatizo kwenye maisha yake akiamini ni siri, lakini anajikuta yote yanasambaa mitaani bila kujua nani kavujisha.

Siku zote siri za mtu hutolewa na mtu aliye karibu naye.

Ndiyo maana watu wa intelijensia wana msemo wao wa 'usimwamini mtu yoyote hata kama ni maiti.' Maiti huwa haizungumzi na wala haijui lolote lile linalotendeka duniani. Lakini badi unaambiwa kuwa usiiamini. Hii ni kukupa msisitizo kuwa hutakiwi kuamini kitu chochote au mtu yeyote kwa siri au mambo ambayo yanatakiwa yawe siri yako.

Filamu ya 'Mfuko Mweusi' ina mtazamo huo, unaowataka watu kuwa makini, kwani unaweza kumwamini mtu, lakini akawa si mtu mzuri.

Inaanzia kwa Bi Staa. Huyu ni mwanamke shugamami. Anampenda kijana mmoja kibenteni.

Binti ya Bi Staa aitwaye Merina anachukia kuona mama yake anatembea na kijana mdogo, lakini anapakiwa maneno ya mama yake.

Mwisho wa siku yalipozidi akafukuzwa




nyumbani ili mama apate nafasi ya kutanua vizuri na kibenteni chake.

Merina anakwenda kuomba kazi kwenye baa. Huko nako kama kawaida anakutana na changamoto kibao.

Huku alikokuacha nako, mama yake akaanza kugombana na kibenteni wake hadi akamtimua.

Kibenteni akanyang'anywa khanga mchana kweupe, ng'ombe anakula majani.

Kwa bahati mbaya sana, Merina akaingia kwenye mapenzi ya mtu mmoja anaitwa Kupa.

Huyu jamaa si mtu mzuri. Ni jambazi, tena mdhulumati. Merina hajui. Kutokana na kuhangaika, akahamia kabisa kwa mpenzi wake huyo.

Kupa akiwa ofisini anapanga mipango ya kwenda kuiba kifuko cheusi. kwa sasa yeye ni mkubwa, anatuma vijana wake kwenda kuifanya kazi hiyo.

Hata hivyo, baada ya kuupata anafanya mpango wa kuwadhulumu wenzake. Hata hivyo mpenzi wake Merina hajui hilo. Siku hiyo anakuja kutekwa na majambazi ili akawaonyeshe alipo mpenzi wake. Kupa anapatikana na Merina akaachiwa.

Hata hivyo, jambazi wa kike papo hapo anataka kumgeuka mwenzake baada ya kuupata mfuko mweusi unaoonekana kuwa una pesa au mali yenye thamani.

Hiyo inampa fursa jambazi aliyekuja naye kumchapa risasi demu yule. Lakini hilo linakuwa limempunguzia kazi Kupa, alimmalizia aliyebakia.

Alichukua mfuko mweusi, akaenda kumkabidhi mpenzi wake Merina. Akamwambia aondoke eneo lile kwani limekuwa ni la hatari. Alipotokomea, aliwasiri jambazi mwingine naye akiutaka mfuko huo weusi. Ngumi zikafumuka, Kupa akamalizia na kutoa bastola akampiga jambazi mwezake, lakini ghafla na yeye akatwangwa risasi ya kichwa.

Ilikuwa ni kazi ya askari polisi ambaye alijitokeza na kuanza kupigia simu wenzake waje wachukue miili ya majambazi waliokufa kwenye mapambano. Kifuko au mfuko mweusi ukawa mikononi mwa Merina aliyerejea kwa mama yake akiwa amenona.



## Mai Zumo mtoto asiyeleta presha

MAI Zumo mwenye umri wa miaka sita, anaweza kuwa mtoto wa kwanza tajiri ambaye anamudu kujilipia ada bila msaada wa wazazi.

Mtoto huyo ambaye anatoka katika familia ya baba Anko Zumo na Habiba Zumo, wenye vipaji vya uigizaji.

"Mai amefanana na bibi yake wa upande wa baba yake, lakini kwa asiyemjua hudhani amefanana na mimi sasa hivi yupo darasa la kwanza ana miaka sita, anaingiza pesa kwa kiasi ambacho yeye anafanya kazi hasa kwa faida yake na maisha yake, sasa hivi anajilipia mwenyewe ada," amesema Mama Mai Zumo.

# MEDIOCRE YA KIBA KUMBE IPO 'LONGI

**Na Adam Fungamwango**

WIKI mbili zilizopita, Septemba 24, msanii maarufu nchini Ali Kiba aliachia ngoma yake kali inayoendelea kutamba mpaka sasa inayoitwa 'Mediocre'.

Hii ni moja kati ya ngoma za vijembe na maneno ya kukerana baina ya wasanii kwa wasanii, ambayo kwa kiasi fulani inasababisha msisimko kwa mashabiki wa muziki huo ambao wanakuwa wanabishana tu barabarani na mitaani kuhusu nyimbo za aina hiyo.

Moja kati ya beti ambazo zinapendwa sana na mashabiki wa bongo fleva ni ule unaosema 'Sichezi na dada zangu nacheza na dada zako, mimi nafanya wimbo, wewe unafanya skendo ili uonekane.'

Kwa mashabiki wa muziki wa dansi nchini, jambo la wanamuziki au bendi kuimbana, kutupiana vijembe si la ajabu kwani limekuwapo tangu zamani.

Wanakumbuka jinsi bendi mbalimbali zilivyokuwa zikiimbana mafumbo na baadaye nyingine inajibu mapigo.

Hizi ni baadhi ya nyimbo za vijembe zilizotamba mno miaka ya 1980.

**Talaka Rejea-DDC Mlimani Park**

Wimbo huu ulitungwa na Shaaban Dede, mara tu baada ya kuihama Msondo na kuingia Sikinde.

Inadaiwa kuwa kijembe hiki aliwapiga Msondo ambao walionekana kutomthamini, lakini alipotaka kwenda Sikinde wakataka kumzuia.

Dede aliimba kwa nafsi ya mwanamke anayemwambia mume wake kuwa alimtaliki na kumnyang'anya nguo mbele za watu, lakini leo anamwambia arejee kwake, lakini yeye anamwambia kuwa hawezi kurejea tena kwake na hamtaki tena.

**Radhi ya Wazazi - Juwata Jazz Band**

Haikujulikana ni mwanamuziki gani aliimbwa kwa sababu hakutajwa jina. Inasemekana hili ni dongo kwenda upande wa pili wa Sikinde. Msondo walitunga wimbo mmoja unaitwa 'Radhi ya Wazazi,' Mtunzi wa wimbo huo ni marehemu Said Mabera aliyefariki hivi karibuni.

Ni kwamba wanamwambia jamaa kuwa wakwe zake wamemchoka, wamechoka kulisha mke na mume. Mtunzi alitunga kama vile yeye ni ndugu wa jamaa huyo anayeishi ukweni.

Amwambia ndugu yake kuwa wakwe wamemfuata nyumbani kumlalamikia kuwa anawabana pale nyumbani, hivyo anamsihi ndugu yake aondoke hapo na mkewe, kwani akufukuzae hakwambii toka.

**Pole Mzee - DDC Mlimani Park**

Ni bonge la dongo lililotungwa tena na marehemu Shaaban Dede. 'Pole Mzee' ni dongo lililoelekezwa kwenye bendi ya Msondo kutokana na wanamuziki wengi wa bendi hiyo kuhama mara kwa mara na kuhamia Sikinde.

Mtunzi anamuuliza hivi jamaa ana kasoro gani hapo nyumbani, kwani watoto wote wamekimbia hapo nyumbani sasa amebaki na wajukuu, ambao ana wasiwasi kuwa nao pia watasambaa baadaye.

Mwisho anampa pole mzee huyo na kusema hiyo yote ni kwa sababu ya tabia yake mbaya.

**MV Mapenzi - DDC Mlimani Park**

Sikinde inaonekana kuwa ndiyo ilikiwa kinara wa nyimbo za vijembe na mafumbo, kwani waliibuka tena na wimbo wa 'Mv Mapenzi' uliotungwa na Mwarami Said. Ni wimbo unaomzungumzia nahodha aliyejitosa baharini baada ya kuona meli imepigwa na dhoruba, lakini baadhi ya mabaharia walitulia na kuifanya meli kusonga mbele baadaye.

Hilo lilikuwa dongo kwa Orchestra Safari Sound (OSS), hasa walimlenga Muhidini Gurumo ambaye alikuwa kiongozi wa bendi, pamoja na baadhi ya wanamuziki, waliihama sikinde na kwenda kwenye bendi hiyo kuanzisha mtindo wa 'Ndekule'.

**Usichezee Chetu - OSS**

Baada ya kuimbwa kwenye 'Mv Mapenzi', Guruma na Hassan Bitchuka nao hawakukaa kimya, nao wakajibu mapigo kwa wimbo wa 'Usimchezee Chatu'.

Wakawaambia kabisa kuwa chatu ni mnyama asiye kivuli, hana mfupa na wanatoa onyo kwa yoyote yule anayemchezea chatu atamezwa na ataukosa ushindi.

Hivyo wamuonya yeyote yule anayemchezea chatu, hatopata kitu zaidi ya kutokewa na ajali na kupoteza maisha yake.





# Tobaa! Card B umelewa au makusudi...

RAPA wa Marekani, Cardi B, ameibua taharuki katika mitandao ya kijamii, baada ya kuachia picha kwa bahati mbaya inayomwonyesha akiwa nusu utupu.

Card B alipiga picha hiyo katika sherehe yake ya kuzaliwa huko Las Vegas, lakini kwa bahati mbaya aliingiza kwenye akaunti ya Istagram na kuibua mshangao kwa mashabiki zake.

Hata hivyo, baada ya kugundua jambo hilo, alifuta haraka na kuwaomba radhi kwa kutumia video aliyoweka mtandao wa Twitter.



## Kanye West apinga Sars

MWANAMUZIKI bilionea wa Marekani, Kanye West, amejiunga na wanaandamanaji wa Nigeria ambao wanapinga kikosi cha kupambana na uhalifu maarufu kama Sars.

Akitwiti akitumia kaulimbiu ya #EndSars, amesema serikali inalazimika kuwasikiliza vilio vya watu wake.

"Nasimama pamoja na kaka na dada zangu wa Nigeria kuwaondoa polisi wanaonyanyasa, serikali lazima ijibu vilio vya watu," ameandika.

## Cobblah kakumbana na wasiojulikana

MSANII wa filamu wa Ghana, Dennis Cobblah, ametoweka katika hali ya kutatanisha.

Katika ujumbe uliosambaa katika mitandao ya kijamii, imeelezwa Dennis ambaye anakuja kwa kasi katika tasnia hiyo, tangu aondoke nyumbani siku tano zilizopita, hajarudi na simu yake imezimwa.

Taarifa zinadai siku hiyo alipanda teksi kwa ajili ya kwenda kukamilisha kazi yake, lakini mpaka sasa hakuna taarifa zozote za kutia moto walizopata ndugu na marafiki zake.






## We Davido huyu baunsa kakufanya nini?

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Davido, amekuwa matatani baada ya kutuhumiwa kumshushia kipigo na kumjeruhi mlinzi wa klabu moja ya usiku.

Taarifa zilizopatikana, zinasema tukio hilo limetokea jijini Abuja, baada ya mwanamuziki huyo na wapambe wake walipojaribu kuingia ukumbini kwa nguvu huku wakimshambulia baunsa huyo.

Katika ujumbe wa malalamiko, mtu aliyepata mkasa huo alimtaka msanii huyo kuwa mwangalifu na matendo yake, ni muhimu kubadilika.

## Swanky afunga ndoa kisiri

MCHEZA filamu nyota kutoka Nollywood, Jideofor Achufusi, maarufu kama Swanky J.K.A, amefunga pingu ya maisha.

Ndoa hiyo ambayo imeelezwa kuwa ya siri, ilifichuliwa baada ya Swanky, kuweka picha ya harusi katika akaunti yake ya Instagram.

"Tafadhali, mimi sio bwana harusi, sasa wote ni waandamanaji," aliandika ujumbe ambao iliwafanya mashabiki wake kuibua mjadala mkali kuhusu ndoa hiyo.



**MAKALA**

# SIMULIZI YA MWENYE ULEMAVU (2)

## ■Nilikosa chanjo nikapata polio, upofu
## ■Ninatamani kuwa mlemavu wa mfano

**Na Mwandishi Wetu**

**NAITWA Eligius Bwalya, mlemavu wa macho na viungo, nilizaliwa Julai, 06, 1986 katika Kijiji cha Muzi kandokando ya Ziwa Tanganyika Wilaya ya Sumbawanga Vijijini ambayo leo inaitwa Kalambo mkoani Rukwa.**

**Mama yangu ananiambia nilipozaliwa nilikuwa mzima na mkamilifu wa viungo vyote, nikiwa mtoto wa saba katika familia ya mama Augustino Mbao na Simon Bwalya, iliyokuwa na watoto 10.**

**Hata hivyo, nililemaa mguu kutokana na polio au pepopunda, kutokana na kukosa chanjo, lakini baadaye nilipofuka na kuondolewa jicho moja wakati moja likiharibika, baada ya kuugua surua. Hii pia ilitokana na wazazi wangu kutonipeleka kwenye chanjo.**

**Imani ya ushirikina ilichangia, wazazi waliamini kuwa nililogwa. Badala ya kwenda hospitali, tiba zilitoka kwa waganga wa kienyeji, hivyo kukuza tatizo.**

**Wiki iliyopita, tulichapisha sehemu ya kwanza ya simulizi la mwalimu Bwaliya, aliyesoma Shule ya Msingi Mlangali na Kaengesa mkoani Rukwa, alimaliza elimu ya sekondari kidato cha tano na sita katika Shule ya Kantalamba na kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), leo tunamalizi simulizi yake inayowahamasisha, kuwaamsha, kuwaasa na kuwatia moyo wasomaji ili kila mmoja awe mhitaji au kiongozi achukue hatua...**



Bwalya: Wenye elemavu tunaweza kufanya lolote na ndilo lengo langu kuionyesha dunia kuwa tunaweza.
**PICHA: MWANDISHI WETU**

WAKATI Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kilipoadhimisha jubilei ya miaka 50, sikusahaulika nilipata medali ya dhahabu ni kutokana na kushiriki kikamilifu michezo ya kuvuta kamba na kuogelea.

Kwa hakika licha ya kuwa na uhitaji nilifurahia maisha ya UDSM na nilihitimu shahada ya kwanza 2013 nilifaulu nikiondoka na alama za GPA ya 3.8.

Katika mazingira ya chuoni kuna watu waliokuwa wananisomea vitabu wanasoma nami nawasikiliza, wamechangia sana kwenye maisha yangu kitaalumu nawashukuru.

Niseme kuwa chuoni na popote kwa wasioona ni vigumu kusoma kama si maandishi ya brail (nukta nundu) hivyo, niwashukuru walionisaidia akiwamo Kjugusi, Donath Marandu na Paul Shiboni kwa kuniongoza na kunisomea vitabu na matini mbalimbali.

**KUANZA KAZI**

Ilipofika Aprili 2014, baada ya kuhitimu ualimu na kupata shahada ya elimu ya watu wazima na maendeleo ya jamii, niliajiriwa kufundisha Sekondari ya Pugu iliyopo katika Manispaa ya Ilala Dar es Salaam.

Shule hii inajumuisha pia wanafunzi wenye ulemavu wa viungo. Mkuu wa Shule J. Mutabuzi alinipokea na kunipatia nyumba ninamoishi mpaka wakati huu, ninamshukuru sana.

Mwezi mmoja na nusu baada ya kupata ajira Mei 25, 2014 nilipata pigo la kufiwa na mdogo wangu aliyekuwa msaada kwangu, kwa kuzaliwa alikuwa ananifuata, ni marehemu Frank Bwalya, aliyeacha mjane na watoto wawili.

Nilimshukuru Mungu kwa vile ni muweza wa kila kitu, lakini ili nipate usaidizi wa karibu, mwaka 2015 nilimuoa Stella Shija tuliyefunga ndoa Desemba 2016, katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Francisco Parokia ya Pugu.

**CHANGAMOTO KAZINI**

Kutokana na ulemavu wangu, nilipata changamoto ya kufundisha ipasavyo kwani kutembea na makabrasha huku nimeshika gongo na fimbo nyeupe ya kuniongoza ilikuwa ni mzigo.

Hali hii ilisababisha Februari 2015 nihamishiwe katika Idara ya Elimu ya Sekondari Manispaa ya Ilala, lakini changamoto za usafiri na kufika kazini kwa wakati ilikuwa ni tatizo kubwa. Suala hili lilinifanya nijiongeze na nikaamua kwenda masomoni kwa ajili ya elimu ya uzamili, Novemba 2015 na niliamua kuchukua shahada ya uzamili watu wenye mahitaji maalumu (Master of Education in Special Education) katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu cha Sebastian Kolowa (Sebastian Kolowa Memorial University) kilichopo Lushoto-Tanga.

Naishukuru Halmashauri ya Manispaa ya Ilala kwa wakati huo , ikiongozwa na Isaya Mgurumi kugharamia elimu yangu ya uzamili lakini pamoja na Ernst Scheifele raia wa Ujerumani, kwa kunisaidia pale nilipokwama kifedha.

Mnamo Mei 30, 2018, dada yangu, Mariana Simon Bwalya alifariki dunia na akatuachia watoto watatu pamoja na changamoto hii, nilihitimu masomo yangu mwaka 2018 na nikapata GPA ya 4.2. Nikiwa katikati ya mwaka wangu wa mwisho wa masomo, mke wangu Stella Shija, aliugua kiasi kwamba ilibidi muda wangu wa kuhitimu masomo ya uzamili usogezwe mbele, yaani badala ya mwaka 2017 nikahitimu 2018.

Nina shukurani za kipekee kwa kaka yangu Kepteni Joseph Wakuwile, kwa kusimama kidete kwa kila hali na mali kwani baada ya muda kuongezeka, sikupata tena msaada wa kifedha kutoka kwa mwajiri wangu kama ilivyokuwa hapo awali. Pia napenda niwashukuru Winfrida Malumbo, Msafiri Diliwa, Joshua Kitale na Rwizza Medard kwa kuniongoza na kunisomea vitabu na matini mbalimbali wakati wa masomo yangu ya shahada ya uzamili.

Niliporudi masomoni, nilibadilishiwa majukumu na kuhamishiwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), ninapofanyakazi hadi sasa kama Mratibu Ukuzaji na Upimaji Mitaala.

**SERIKALI IMENISIMAMIA**

Hayo yote yamefanikishwa na Katibu Mkuu Kiongozi John Kijazi, aliyeeleza hali na mahitaji yangu kwa Katibu Mkuu Utumishi, Profesa Laurean Ndumbaro, baada ya kumweleza changamoto zangu za ulemavu na utendaji wa kazi na hatimaye nikaletwa hapa NACTE.

Ninamshukuru Katibu Mtendaji wa Baraza la NACTE A. Rutayuga, na wasaidizi wake wote kwa kunipokea na kuhakikisha napata mahitaji yangu muhimu ya kuniwezesha katika utendaji wangu ikiwa ni pamoja na usafiri.

Changamoto zipo ila naamini kwa kushirikiana na watawala wangu zitakwisha kabisa kwa kadiri zinapotokea na kwa bahati nzuri muda wote wako tayari kunisikiliza, kuzipikea na kuzitatua pale ninapowaeleza.

**NINACHOKITAMANI**

Ni baba wa familia mwenye watoto watatu japo nipo katika harakati za kusaka ufadhili kwa ajili ya masomo ya uzamivu (PhD) kwani ndoto yangu haijatimia.

Natamani niwe mfano wa walemavu wenye ulemavu zaidi ya mmoja ili kundoa mawazo kwa walemavu wa aina hii na wazazi na jamii kwa ujumla wenye mtazamo hasi dhidi yetu kuwa walemavu hatuwezi kitu kwa sababu ya hali tuliyo nayo kimaumbile.

Naomba nimalize kwa kuwashukuru vijana wawili ambao kwa kipindi chote hicho wamekuwa msaada kwangu nilipokuwa nje ya masomo, wao walikuwa jicho na miguu yangu. Ni Beda Mpepo na Mohamed Ahmed; hakika wamekuwa nguzo katika maisha yangu na Mungu awabariki mno. Kwa sasa ninaishi na kijana anayenisaidi ambaye ni Emily Jabir.

**SOMO LA SIMULIZI**

Huu ni ujumbe wangu, naomba tujifunze katika mapito yangu, Eligius Bwalya, ujueni kuwa ulemavu si sababu ya kutofikia malengo na ndoto zetu.

Kadhalika iwapo kutakuwa na mazingira rafiki, watu wenye ulemavu wanaweza kufanya mambo sawa na wasio na ulemavu na pengine zaidi yao.

Aidha, wazazi na walezi wasiamini sana ushirikina na kusahau matibabu ya hospitalini kwani inaonyesha wazazi wangu Bwalya walishindwa kunipeleka hospitalini kwa ajili ya chanjo ya magonjwa ya utotoni yakiwamo polio na surua.

**SOMO KWA WALEMAVU**

Kadhalika, simulizi yangu inawapa ujumbe wenye ulemavu kuwa hawapaswi kukata tamaa kwa sababu yoyote ile, mfano mtazamo hasi kutoka kwa jamii kuwa hatuwezi kitu kutokana na ulemavu.

Aidha, wazazi na walezi wasiwafiche watoto wenye ulemavu wakidhani kuwa hawana maisha tena kisa ni walemavu, wakumbuke wakati mwingine ulemavu ni fursa. Watunga sera na miongozo mbalimbali wazingatie mahitaji maalumu ya walemavu na tukumbuke kuwa ulemavu si ugonjwa bali ni hali ambayo mtu anapaswa kukubaliana nayo. Kwani atafanya juhudi za kukabili changamoto zitokanazo na hali hiyo ya ulemavu.



Soko la kisasa linalojengwa chini ya mradi wa Dar es Salaam Metropolitan Development Project (DMDP), jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MAELEZO**

# Ulivyo mradi unaogeuza jiji la Dar yenye sura mpya, makuu yanakuja

## ■Umeshameza mabilioni, zingine zasubiri

**Na Mary Geofrey**

DAR ES SALAAM ndio jiji kubwa kitaifa, siyo jana hata leo, bali una muda. Kila kukicha ni mbadiliko ya kila aina. Vitongoji pori vya kale kama Buza, Kibada, Mbezi, Bunju na Kinyerezi zama hizo za miaka ya 1980, leo hii ni maeneo maarufu.

Jiji limeshapanuka na kuboreshwa sawasawa. Leo hii kuna awamu ya kwanza ya kinachoitwa Mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam (DMDP), katika Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke, ukifadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) na unakadiriwa kugharimu Sh. bilioni 660.

Mradi huo uliofikia hatua ya asilimia 80 tangu kuanza mwaka 2015 na utakamilika mwakani, unajumuisha ujenzi wa barabara, vituo vya mabasi, masoko, mifereji ya majitaka, madaraja na vyoo.

Humphrey Kanyenye, Mratibu Mkuu wa Mradi wa DMDP, anasema mbali na kasi walio nayo kutekeleza, wanakabiliwa na vikwazo kadhaa kama vile msongamano na ongezeko la watu mitaani na hali ya hewa mbaya, ikiwamo mvuia kubwa.

"Tunatarajia kukamilisha kazi hii kwa wakati kama ambavyo awamu ya kwanza inatakiwa kukamilika kwa asilimia 100," anasema Kanyenye, anayedokeza awamu ya mwisho inatarajiwa kumalizika mwakani 2025.

**TEMEKE YABORESHWA**

Mratibu wa mradi DMDP Temeke, Edward Simon, anachangia katika eneo lake kwamba limegawanyika katika vipengele 15, akiainisha baadhi ujenzi wa barabara za Kijichi-Tuangoma, Mwanamtoti na penye ofisi ya mradi.

Pia, anataja barabara za Chang'ombe Mchicha na Temeke Mbagala, ujenzi wa Bonde Gerezani, maboresho ya bonde la Mto Kizinga na miundomboni ya jamii katika kata ya Kilakala na Keko.

Anaainisha bajeti yake kwamba: "Halmashauri ilitarajia kupokea Sh. bilioni 265 na imechangia Sh. bilioni 20.3 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa miundombinu hadi Julai mwaka huu."

"Halmashauri imepokea jumla ya Sh. bilioni 148 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika maeneo hayo," anaeleza Simon, anayetaja manufaa ya miradi umepunguza foleni za magari barabarani, kupungua mafuriko ya mvua, usalama utokanao na taa barabarani, ajira.

Vivyo hivyo, Simon anataja vyanzo vipya vya mapato katika manispaa, akidokeza katika kipindi cha miezi sita pekee, vya halmashauri imekusanya zaidi ya Sh. milioni 400 katika masoko na vituo vya mabasi vipya, chii ya mradi wa DMDP.

**KINONDONI INAPAA**

Mratibu wa DMDP Manispaa ya Kinondoni, Mkelewe Tungaraza anasema, watekeleza miradi ya kujenga miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami, usimikaji taa za barabarani zinazotumia nguvu ya jua, kujenga njia za watembea kwa miguu na mifereji ya maji ya mvua.

Anataja miradi mingine ni vyoo vya umma, viwanja vya mipira, masoko na sehemu za kupumzika katika maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Kinondoni na manispaa mpya ya Ubungo, iliyokuwa awali sehemu ya Kinondoni.

Kuhusu malengo, anasema ni katika uboreshaji miundombinu ya barabara na mifereji ya mvua, kuimarisha uwezo wa taasisi kukusanya mapato na kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi moja na kupunguza athari za mafuriko.

Anasema, katika utekelezaji mradi hiyo, imegawanywa katika sehemu tisa na utekelezaji wake upo katika hatua za ukamilishaji kabla ya mwaka ujao, hapo akiorodhesha mambo kadhaa.

Tungaraza anayataja kuwa ni ujengaji barabara kiwango cha lami kwa urefu wa kilometa 7.58, mifereji mikubwa ya maji mvua mita 780, kuwekaji taa 196 barabarani na njia ya watembea kwa miguu, zote zitakapokamilika, zinatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 19.2

Zingine zinahusu barabara ya kiwango cha lami, urefu wa kilomita 10.65; mifereji ya maji ya mvua na njia za watembea kwa miguu kwa zote zikigharimu Sh. bilioni 28.9.

Msimamizi huyo wa mradi, anasema kuna barabara za kati ya Korogwe - Kilungule hadi Maji Chumvi yenye urefu wa kilometa 5.73 zinazojengwa kwa kiwango cha zege; barabara ya External-Jeshini, kilometa 1.3 kiwango cha lami; na barabara ya Kisukuru-External, urefu wake kilometa 3.2 zikiwa na taa zinazotumia nguvu jua, mradi kwa jumla ukutumia Sh. bilioni 21.59.

Kadhalika anasema, wamejenga kingo za mto Sinza kilometa 9.774 na mfereji wa Kiboko kilometa 3.5, iliyowekewa kingo za zege, sambamba na kujenga mabwawa mawili ya kuhifadhi maji; vivuko 12 vya watembea kwa miguu na makalavati matano.

**ILALA MPYA**

Manispaa ya Ilala nayo ina yake, Mratibu wa DMDP, Mhandisi Selastina Rwegasira, akisema walitengewa bajeti ya Sh. bilioni 115 kuwezesha kuboresha miundombinu na kupanua uwezo wa manispaa.

Hapo Mhandisi Selastina, anafafanua katika utekelezaji mradi, imelenga kujenga barabara za lami kilometa 41.11; ghorofa moja; maabara ya mradi; vituo vinane vya kukusanya taka ngumu; masoko matatu; na maeneo ya mapumziko mawili.

Pia, anataja nia ya kuwa na mifereji mikubwa ya maji ya mvua kilometa 15.96; vyoo vitatu vya umma; kuchimba visima nane; na kujenga vizimba sita vya maji safi; pia visima vyenye pampu ya mkono.

Anafafaua: "Serikali inawajibika kulipa fidia kwa wananchi wanaoguswa na mradi kwa kuwa mradi unaotekelezwa kwenye maeneo yasiyopangwa kwa kiasi kikubwa."

Kwa mujibu wa mratibu huyo wa mradi katika Manispaa Ilala, hadi sasa jumla ya Sh. bilioni 11,354, zimeshalipwa fidia kwa wananchi 1,265, katika mchanganuo serikali ilitoa Sh. bilioni 9.3 na halmashauri kwa mapato ya ndani Sh. bilioni mbili.

Anaeleza mradi wa DMDP Ilala, umegawanywa katika mafungu saba, anayoyataja ni: Ujenzi wa barabara za lami kilomita 2.8 kwa barabara nne.

Mhandisi Selastina anasema, hadi tarehe 30 ya mwezi uliopita, kuna jumla ya kilometa 30 za barabara zimeshajengwa na zinatumika, zikibaki kilomita 11 kumaliziwa.

Pia, anataja asilimia 99 ya kukamilika kwa masoko matatu na vyoo vya umma viwili, kati ya vitatu vilivyolengwa; visima vinane vya maji safi, kati yake sita ni vya kutumia pampu za umeme na vyenye vizimba sita.

Aidha, kuna visima viwili anavitaja vyenye pampu za mkono vimeshakamilika na vinatumika na vitatu vya kukusanyia taka ngumu vimeshajengwa; mifereji mikubwa ya maji ya mvua kilometa 9.55 imeshakamilika, kati ya kilometa 20 inayolengwa.

"Fedha zilizotumika hadi sasa ni Sh. bilioni 66. 6 kati ya Sh. bilioni 115 zilizotengwa na miradi hii yote ipo mbioni kukamilika," anahitimisha Mhadisi Rwegasira.



Barabara iliyojengwa wilayani Temeke, kupitia mradi wa Metropolitan Development Project (DMDP).

# DRC yakabiliwa tishio la njaa

**KINSHASA, DRC**

SHIRIKA la Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), limetangaza zaidi ya watu milioni 22 wanakabiliwa na ukosefu wa chakula nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Mwakilishi wa shirika hilo nchini DRC, Aristide Ongone Obame, alisema sababu zilizochangia hali hiyo ni vita vya kikabila na migogoro inayotokana na kuimarika kwa vikundi vinavyomiliki silaha. Taarifa hiyo inatokana na utafiti wake unaofanyika kila mwaka.

Obame, aliliambia Shirika la Utangazaji ya Ujerumani (DW), kuongezeka kwa kasi kwa idadi ya watu wanaokabiliwa na baa la njaa ni kutokana na kuongezeka kwa janga la Covid-19 katika mikoa 21 ndani ya nchi hiyo.

Alisema "Hatua zote zilizochukuliwa na serikali za kuruhusu safari kati ya mikoa hapa nchini, baadhi ya maeneo yanakosa huduma kutoka Kinshasa.

Baadhi ya athari zilizotokana na kuenea kwa virusi vya corona nchini DRC ni kukwama kwa shughuli nyingi za kiuchumi kusimamishwa zikiwamo na shule za msingi na sekondari.

Hata hivyo, serikali iliamua mwanzoni mwa wiki hii. Kufunguliwa kwa shule baada ya miezi sita bila masomo.

Mkuu wa Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa, (UNESCO), Audrey Azoulay, yupo katika ziara nchini humo kukagua mazingira ya shule na jinsi wanafunzi watakavyorejea shuleni.

Bi Audrey, alisema UNESCO litaunga mkono utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo ambayo imeruhusu watoto wengi kwenda shuleni.

**DW.**



Watoto kutoka jamii ya Rohingya, wakioga maji ya mto kambi ya wakimbizi ya Kutupalong, Ukhia nchini Bangladesh. **(PICHA: AFP)**

# Trump, Biden washambuliana wakiwa tofauti

**WASHINGTON, Marekani**

WAGOMBEA wa kiti cha urais nchini Marekani, Donald Trump, kutoka Republican na Joe Biden anayewania kupitia Democratic, wameshambuliana katika mdahalo uliofanyika kupitia vituo viwili tofauti vya televisheni.

Katika mdahalo huo, kila mmoja amemtuhumu mwenzake, kuhusu namna anavyouchukulia ugonjwa wa COVID-19, sambamba na siasa za ndani na za kimataifa.

Watu wengi wameelezea mahojiano hayo kama duru ya pili ya mdahalo wa uso kwa uso kati ya Trump na Biden, baada ya ule wa awali uliopangwa kufanyika juzi baada ya Trump akajitoa kutokana na waandaaji kuamua ufanyike kupitia mtandao. Uamuzi wa kutumia mtandao ulitokana na Rais Trump kuugua ugonjwa wa COVID-19 wiki mbili zilizopita.

Akihojiwa na kituo cha televisheni cha ABC mjini Philadelphia, Biden, alisema Trump hajachukulia kwa umakini maradhi hayo, ambayo yamewaangamiza Wamarekani zaidi ya laki mbili.

**DW.**

# Serikali, waasi Yemen kubadilishana wafungwa

**SANAA, Yemen**

MAZUNGUMZO ya kumaliza vita vinavyoendelea nchini Yemen, yamefikia hatua muhimu ya ubadilishaji wa wafungwa 700 wa kivita wanaoshikiliwa kila upande. Operesheni kubwa ya ubadilishanaji wa wafungwa katika mgogoro huo uliwahi kufanyika miaka mitano iliyopita.

Shirika la Kimataifa la Msalaba Mwekundu, lilisema juzi kwamba limefanikisha kusimamia uhamisho na kuachiwa kwa zaidi ya wafungwa 700.

Uhamisho huu wa wafungwa unafanyika miaka miwili baada ya makubaliano kufikiwa kufuatia mazungumzo yaliyosimamiwa na Umoja wa Mataifa nchini Sweden mwezi Desemba. Kulingana na vyombo vya habari vya waasi wa Kihouthi, ndege itakayowabeba karibu wafungwa 150 imetua katika uwanja wa ndege wa Sana'a jana ili kuwapeleka katika makao ya muda ya serikali inayoungwa mkono na Saudia Arabia, katika mji wa Aden uliopo kusini mwa Yemen.

**DW**

# Waziri Mkuu Thailand aapa kubaki madarakani

**BANKOK, Thailand**

WAZIRI Mkuu wa Thailand, Prayuth Chan-ocha, ameapa kutoachia madaraka baada ya kusambaa kwa maandamano kwa ajili ya kuipinga serikali yake.

Maelfu ya waandamanaji wanaoipinga serikali waliendelea kubaki barabarani kama njia ya kukaidi agizo la serikali inayotaka watu kuacha kuandamana.

Maandamano yaliyofanyika juzi jioni yalikuwa makubwa kuwahi kufanyika katika mji mkuu wa nchi hiyo, Bangkok.

Kutokana na shinikizo hilo, kikao cha dharura cha baraza la mawaziri kilichoongozwa na Prayuth kilifanyika na amewaambia waandishi wa habari kuwa hatojiuzulu."Serikali lazima itumie amri ya dharura. Lazima tuendelee kwa sababu hali ilikuwa mbaya. Amri hii itaendelea kutumika kwa siku 30 au kama machafuko yatapungua basi itatumika kwa siku chache."Marufuku ya mkusanyiko wa watu zaidi ya watano yaliwekwa mapema jana baada ya karibu miezi mitatu ya maandamano. Maandamano hayo ni ya kutaka kupunguzwa kwa mamlaka ya utawala wa kifalme wa Mfalme Maha na pia kuondolewa mamlakani kwa Waziri Mkuu Prayuth.

**DW**

# Boris Johnson njia panda Brexit

**LONDON, Uingereza**

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, yupo njia panda kuamua hatua nyingine itakayochukuliwa na nchi yake katika mazungumzo na Umoja wa Ulaya (EU), kuhusu uhusiano wa kibiashara.

Hatua hiyo itakuwa ya pili, baada ya ile ya awali kutopata mafanikio baada ya mazungumzo hayo kutakiwa Uingereza ijiandae kuondoka bila makubaliano, licha ya kuwapo kwa hofu ya kuathirika kiuchumi kama itakachukuliwa uamuzi huo.

Miezi minane baada ya Uingereza kujiondoa rasmi kutoka kwenye Umoja wa Ulaya, hakujaonekana mwanga wa kupatikana kwa maelewano kabla kufikia mwisho wa mwaka huu.

Pande zote mbili zimeeleza kuvunjwa moyo kwa kutopiga hatua katika mazungumzo hayo, lakini dalili zinaonyesha yatarefushwa muda wa mwisho.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**DEREVA NA MAUZO**, KATIKA KAMPUNI YA MAJI NAFASI 8 0767 – 269677.

## NYUMBA/VIWANJA NA MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA IKO KAHAMA** MAJENGO VYUMBA VITATU INA MAJI NA UMEME, PLOT No 759, BLOCK "E", KIWANJA NI MEDIUM SIZE. MAWASILIANO ZAIDI; 0759359933/0713553819

**Nyumba self container** ina fence maji na umeme inapangishwa ipo Segerea kwa bibi bei 1,800,000 kwa nusu mwaka 0754467237/0754284708

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA NA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL)** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumaliza tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga: **0758 112 332. Karibu EFL**

**VISIMA DAR NA PWANI:** SASA UTACHIMBIWA KISIMA KWA KILA MITA 1 KWA SHS.75,000/= TU PAMOJA NA pampu.kwa mwezi huu wa oktoba tu. Tupigie 0654291766 /0786687405.

---

### KUPOTEA KWA CHETI



**MARTIN MATHIAS KESSY** anatangaza kupotelewa kwa cheti chenye index No **S-0-130-20** mwaka 1990 shule ya MAUA SEMINARY cha kidato cha nne,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa **DAR/GOG/RB/734136/2020**

115947202

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ESTHER JULIUS MASELE** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI AINA YA **TOYOTA NOAH** YENYE NAMBA ZA USAJILI WA NAMBA **T604 BTM.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLSI. TAARIFA YA POLISI **DOD/DOD/RB/731529/2020.**

115948402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo KIMAMBA.**

**Usimamizi wa mirathi No;07/2020**

**Ombi la SALUMU RAJABU TONYOKE ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RAJABU SALUMU TONYOKE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 23/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 23/09/2020.

Sahihi ya Hakimu
MAHAKAMA YA MWANZO KIMAMBA

115948202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 290/2020**

**Ombi la MARIETHA THOMAS NKINGWA ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SALOME THOMAS LUNEMYA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 16/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 24/09/2020.

Tarehe 24/9/2020
Sahihi ya Hakimu

115948102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO DODOMA MJINI WILAYA DODOMA**

**MADAI NAMBARI 206/2020**

**MDAI HONEST DIONIS MASSAWE**

**MDAIWA MICHAEL SAROTA NYAMONGE**

**Kwa MICHAEL SAROTA NYAMONGE**
**BUNJU- DSM**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA TSH 13,000,000/=.**

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku JUMATANO tarehe29/11/2020 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Na kama haukuhudhuria siku tajwa tajwa hapo juu, Mahakama itathibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kwa kuwa umeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo16/10/2020.

HAKIMU WA MAHAKAMA YA MWANZO.

115948302

### KUPOTEA KWA CHETI



**EVERLINE EPHATA MSANGI** anatangaza kupotelewa kwa cheti na transcript kilichotolewa na chuo cha MWALIMU NYERERE mwaka 2017 index Na **MNMA/BTC.BA10053116** Yeyote atakayekiona atoe taarifa polisi Polisi Taarifa **9910819191290.**

115947702

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHILDREN FOR CHILDRENS FUTURE CCF**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Landcruiser yenye namba za usajili **T 567 AJT,** Yenye chassis namba **L J 790010599** na Injini namba **3L3771145**
Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**MOS/TR/RB/1783/2020**

115947302

### TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya **BEIFANG MINING SERVICES LIMITED** iliyokuwa inapatikana maeneo ya Oysterbay Plaza, barabara ya Haile Sellassie Dar es salaam, wanapenda kuutangazia umma kuwa Kampuni yao yenye namba ya usajili **134389** imefungwa kuanzia tarehe **04/04/2018.**

115947602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA J/PCF.49**

**HATI YA KUUZA MALI YA KUTIMIZA HUKUMU (MCA/84)**

**Mahakama ya mwanzo ya DODOMA MJINI Wilaya DODOMA.**

**Shauri la Madai No.46/2020**

**Madai KISA MKINGA**

**Amdai**

**Mdaiwa FUNGU HASSAN**

**Kwa ROYAL RUNNER'S CO.LTD DODOMA K.K HAKIMU MFAWIDHI MAHAKAMA YA WILAYA S.L.P 923 DODOMA.**

Hati hii ya KUAMURU kuuza katika Mnada wa Hadhara Tarehe 23/10/2020 saa nne asubuhi, baada ya kutangaza kwa muda wa siku 21 kwa kubandika tangazo hilo katika nyumba ya mahakama hii, ikieleza wakati na mahali patapofanywa mnada huo na mali itakayouzwa, na baada ya kutangazwa mali hiyo NYUMBA ILIYPO NZUGUNI 'B' DODOMA iliyokamatwa kwa hati kukamatia mali iliyotolewa na mahakama hii Tarehe 30/07/2020 kwa kutimiza hukumu ya mdai aliyetajwa hapo juu katika shauri hilo juu, au mali itakayo kamilisha idadi ya shilingi 3,700,000.
UNAAMRIWA tena kurudisha hati hii kabla ya tarehe 17/10/2020 ikiwa na maandishi yako kuthibitisha namna ilivyotimilizwa; au kwanini haikutimilizwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 17/09/2020.

115947002

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

# Mauaji Harusini-34

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.
Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.
Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.
Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**

KAMA umeme, alitoka sehemu aliyojificha. Wakati mwenye bastola alishtuka pembeni yake kuna nini, kwani alikuwa akiangalia zaidi mbele, alijikuta akipigwa teke mkononi ambalo lilirusha bastola juu, ikagonga juu na kuanguka chini. Ilikuwa kama sinema hivi. Eddy aliipiga tena teka bastola, ikaserereka na kuingia uvunguni mwa kochi. Ilionekana jamaa mrefu alikuwa yuko vizuri, kwani alirusha teke ambalo Eddy aliliona vizuri na kulipangua kwa mkono.

Kwa sababu jamaa hawakuwa tena na bastola, Eddy hakuwa na haraka, wakati akirusha ngumi aliikwepa.

Wakati huo, jamaa aliyekuwa anataka kuingia ndani aliahirisha na kurejea kumsaidia mwenzake.

Huyu ndiye Eddy alianza naye, kwani alijikuta akipigwa teke la mbavu lililomfanya aanguke chini kama gunia.

Mwingine alikuwa mbishi alizirusha mbili tatu, huku akiwa hajapigwa hata ngumi moja.

Eddy alitishia kama anapiga ngumi ya kushoto, akawepa kwenda kulia, huko ndiko alikokutana na ngumi na mkono wa kulia iliyomrusha na kichwa chake kujipigiza ukutani.

Taratibu alishuka chini na kuegemea ukutani huku akiwa amekaa.

Eddy alimfuata na kumtazama, akagundua kuwa hakuwa na maisha. Hakuhangaika naye. Alimgeukia mwingine aliyekuwa anagaagaa. "Wewe ni nani na umefuata nini?" Aliuliza.

Hakujibiwa. "Nyinyi ni akinanani na nani amewatuma kuja hapa?" Aliuliza lakini safari hii kwa hasira.

Mlango ulifunguliwa, Shani alitoka. Alichokiona kilimfanya apige kelele za woga kwa sauti kubwa na kurejea alikotoka, akisahau kabisa kufunga mlango.

Eddy hakuhangaika naye, alichofanya ni kuchukua kamba aliyokuja naye jamaa yule na kumfunga mikononi na miguuni. Aliporidhika alimgonga sehemu ambayo alijua atazirai muda wa robo saa hivi kabla ya kuzinduka.

Alienda chumbani kwa Shani na kumkuta amejikunyata kitandani akilia.

Alimkumbatia na kumbembeleza. Shani sasa aliamua kulala kwenye miguu ya Eddy ambaye alipofika alikaa kwenye kitanda.

"Usiwe na hofu mpenzi wangu, tuko salama." Alisema Eddy huku alimpetipeti kwa mikono na busu juu.

"Eddy mimi sielewi nini kimetokea?" Aliuliza huku akiendelea kulia.

"Nadhani ni vibaka waliingia. Walikuwa na nia ya kuiba."

"Ikawaje?"

"Niliwahi kuwaona, nikajificha, wao wakaingia hawakuniona, nikawavamia na kuwapiga kwa nyuma, wote wawili wakaanguka chini." Eddy alidanganya.

Ni kweli aliwapiga. Lakini alitengeneza mazingira ya kumwaminisha Shani kuwa aliwapiga kwa kuwavizia na si kwamba aliwatandika kama fundi wa sanaa za mapigano.

Ukweli ni kwamba bado Eddy hakutaka kumuambia lolote baya, au kama kuna watu anaosaka kutoa roho yake. Lengo ni kumfanya aendelee kuwa na amani na furaha, badala ya kuwa na hofu, wasiwasi na huzuni.

Ndiyo maana alianza kwa kumwambia kuwa walikuwa ni vibaka waliingia.

Eddy pia alikuwa ana kazi ya kuficha ukweli kuwa yeye ni mpelelezi maarufu nchini mwenye ujuzi wa hali ya juu, hivyo alitaka Shani aamini kuwa aliwavizia vibaka wale na hakuwa na ujuzi, au nguvu za kuwapiga.

"Lakini Sherry? Mbona huku hakuna vibaka?"

Lilikuwa ni swali zuri kwa Shani, lakini halikuwa zuri kwa Eddy. Lilienda kukabiliana na ukweli.

Mbezi Beach na mambo ya vibaka ilikuwa ni vitu viwili tofauti.

Ni sehemu ambayo nyumba nyingi zinajitegemea zenyewe. Kila nyumba ina ukuta, tena wenye ulinzi imara.

Ukiona mtu ameingia kwenye nyumba za huko ambazo ni za gharama ujue si kibaka wala mwizi, ila ni jambazi hatari mwenye mafunzo, au mtu aliyetumwa kutelekeza kile alichoagizwa na lazima uwe mtu mwenye uwezo wa hali ya juu katika mambo ya kutumia silaha, kukabiliana na vikwazo kama ukuta wa aina yoyote ule uwe na waya, miba au umeme. Kifupi ni mtu hatari.

"Kwa sababu hatujajua nia yao ni nini, basi lazima tuwaite ni vibaka." Alijibu Eddy baada ya kuona jibu lolote zaidi ya hilo linaweza kuzua maswali mengi.

Baada ya muda mrefu kidogo kumbembeleza mpenzi wake hadi kuonekana amerejea kidogo kwenye hali ya kawaida hadi kupata usingizi, Eddy alitoka varandani na kumkuta jamaa amezinduka.

"Unaitwa nani?"

Hakujibu chochote, alibaki akimwangalia.

Kwa uzoefu wake, aligundua kuwa hakuwa kibaka wala mwizi, ila alikuwa ni mtu mwenye mafunzo maalum, kwani mara nyingi huwa hawana wasiwasi wanapokamatwa na huwa wanafundishwa kutojibu lolote.

Aliinua simu na kuanza kuongeza.

"Nipo Mbezi Beach hapa nyumbani namba 707. Imevamiwa na watu wawili, mmoja ameuawa na mwingine mzima. Kwanza kabisa pigeni simu polisi waje kuuchukua huu mzoga hapa, halafu wewe Pius, tafuta wengine wawili hapo ofisini mje mumchukue huyu jamaa kwa ajili ya kumfanyia kazi fulani ambavyo nitaitaka. Usisahau pia kuwapigia wale jamaa zetu, watupe watu wanne ambao nataka waje kuilinda hii nyumba sawa?"

Baada ya kumaliza kuongea alizima simu yake. Lakini alichogundua kwa mbali ni mshangao na uoga alioanza kuonyesha jamaa yule aliyefungwa.

Maneno yaliyokuwa akiongea Eddy alimfanya kuanza kuhisi kuwa kumbe mle ndani alikuwa akicheza na mtu ambaye si wa kawaida. Si tu mjuzi kwenye mambo ya mapigano kama alivyodhani, lakini pia ama ni ofisa wa polisi, au mtu mwenye cheo cha juu kwenye mambo ya ulinzi wa nchi.

"Hutaki kuongea ee, basi endelea kukaa tu hapo."

Eddy hakuwa na wasiwasi naye, kwani alimfunga madhubuti, lakini kichapo alichompa kilimnyong'onyesha, hivyo hakuwa na nguvu.

Alirejea chumbani na kwenda kumuasha mpenzi wake Shani.

"Ilikuwa uhame wiki ijayo hapa, lakini haiwezekani, leo hii hii utahama na kuhamia kwangu. Hapa si salama tena."

Sauti ya Eddy ilipenya masikioni mwa Shani. Ni kweli aliingiwa na woga, ingawa hakujua vibaka wale nia yao ilikuwa ni kuiba nini mle ndani.

Ni Eddy tu aliyejua kuwa kama siku ile asingekwenda nyumbani kwa Shani, basi asingemuona tena maishani.

Mwili ulimsisimka. "Sijui ingekuwaje?" Alijiuliza. Tangu alipoonana na Shani alitokea kumpenda na hakutaka kitu chochote kile kitokee cha kumtenganisha naye.

Ni mwanamke ambaye amembadilisha kuwa mwanaume wa kwenda kustarehe kwenye mahoteli na mabaa na wanawake warembo wa kila aina, hadi kuwa mwanaume mwenye kupenda na kujali.

Urembo wa msichana yule mdogo tu wa miaka 23, pamoja na misukosuko ya hatari anayopitia bila yeye kujijua, ilimfanya Eddy kumuonea huruma, ikiwemo kuzidi kumpenda na kuwa naye karibu.

Na ndiyo maana awali alimwambia atakuwa akija nyumbani kwake kumchukua, kumpeleka na kumrudisha nyumbani kila asubuhi na jioni, tena akitumia gari lake, badala ya gari la msichana huyo ambalo aliona watesi wake watakuwa wanalifahamu na kulifuatilia.

Alichofanya Eddy ni kulichukua Land Cruiser la Shani na kulificha nyumbani kwake Kijitonyama.

Na hii ni baada ya kugundua kuwa kuna watu wanatafuta kumuua kwa sumu ambayo angeila kwenye chakula siku ile ABC Hotel kama yeye asingegundua hilo.

Leo kuna watu wamevamia nyumbani kwake. "Nadhani lengo ni lile lile kumuua." Alijiambia.

"Ni kweli mpenzi. Kwa hali hii mimi siwezi kukaa hapa na kulala peke yangu." Alijibu kwa sauti ya upole.

"Ningeweza kusema mimi nikae hapa na wewe kwa sababu wote hatutokuwa salama, lakini nadhani itakuwa si vizuri sana, twende kwangu ukakae kwa usalama zaidi hapo tutapokuwa na uhakika wa usalama wetu."

Ving'ora vilisikika na magari matatu yaliwasili hapo. Eddy alitoka kwanza na kwenda kuongea nao nje. Alipoingia aliwaruhusu baadhi ya watu kuingia ndani. Kuna waliochukua maiti ya aliouawa na kuondoka nayo kwa gari la wagonjwa. Jamaa aliyepona alichukuliwa na gari lingine, huku watu wanne wakibaki kulinda nyumba.

"Sherry hawa ni walinzi ambao watakuwa wakiilinda nyumba hii muda wote ambao hatupo. Sasa na sisi naona tujiandae kuondoka, kusanya ambacho unachoweza kukitaka kutumia kuondoke."

Hii ya walinzi ilishangaza kidogo Shani, lakini kutokana na mambo yalivyokuwa, hakutaka kujiuliza sana zaidi ya kujiandaa

"Haya Sherry ngoja nijiandae."




***ITAENDELEA JUMAMOSI***



# MBAPPE

## AFIKIRIA KWENDA MADRID

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe anafikiria kujiunga na Real Madrid ya Hispania.

Kwa mujibu wa ukurasa wa mbele wa gazeti la AS la jana Ijumaa, Mbappe kwa sasa akili yake yote imeelekea Real Madrid.

Huku akiwa anahusishwa kwa muda mrefu na Real Madrid, Mbappe pia amekuwa akiwindwa na Barcelona na Liverpool.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Mbappe anaamini atajiunga na Real Madrid baada ya kumalizika kwa mkataba wake na PSG mwishoni mwa msimu ujao.

Licha ya kuwaniwa na timu kadhaa, lakini Mbappe mwenyewe ameonyesha kuwa Real Madrid ndio sehemu itakayomfaa zaidi kwenye kucheza.

Mbappe ameripotiwa kutokuwa tayari kusaini mkataba mpya na PSG, ambapo unamalizika mwaka 2022.

# HATIMAYE

## OZIL KUONDOKA ARSENAL




**LONDON, England**

MESUT Ozil anaweza kuondoka Arsenal wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari, kwa mujibu wa gazeti la Dail Mail.

Ozil kwa sasa hana namba kwenye kikosi cha Arsenal baada ya Kocha Mikel Arteta kuonyesha hayupo kwenye mipango ya kumtumia.

Arteta anaamini mchezaji huyo haendani na mifumo yake hali inayosababisha asimpe nafasi ya kucheza ikiwa msimu uliopita amecheza mechi 23 tu katika michuano yote.

Mbali na kuonekana hana nafasi ndani ya Arsenal, klabu nyingine zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili zikiamini anaweza kuzisaidia zikafanya vizuri. Kwa mujibu wa ripoti, Ozil sasa anaweza kwenda kucheza soka nchini Marekani katika Klabu ya DC United, ambayo imeonyesha kuwania saini yake.

Klabu nyingi za Ulaya zinagwaya kumsajili Ozil kwa sababu ya mshahara wake mkubwa wa pauni 350,000 kwa wiki, ambao analipwa pale Arsenal.

Licha ya kipindi cha majira ya joto Ozil kuhusishwa sana na mpango wa kuondoka pale kwenye dimba la Emirates, lakini yeye mwenyewe alionyesha kutokuwa na nia ya kuondoka hadi mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.




# BARCA YAMFUNGIA KAZI PAUL POGBA

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona imeonyesha nia ya kutaka kumsajili kiungo wa Manchester United, Paul Pogba.


Kwa mujibu wa gazeti la AS, Barcelona wapo tayari kumsajili Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 27, katika dirisha lijalo la majira ya joto, ili kuboresha safu yao ya kiungo, ambayo inaonyesha kupwaya.

Hata hivyo, usajili wa Pogba unaweza kukamilika kama Ousmane Dembele atakubali kwenda United ikiwa sehemu ya mabadilishano ya wachezaji.

Barca kwa sasa imeyumba kiuchumi hali inayosababisha ishindwe kufanya usajili kwa kutumia fedha nyingi, hivyo, ili kuhakikisha inaipata saini ya Pogba italazimika kumwachia Dembele, ambaye United inaitamani saini yake kwa muda mrefu na dirisha lililopita dili hilo lilishindikana dakika za mwisho.

Mkataba wa Pogba unatarajiwa kumalizika mwaka 2021 na thamani yake katika soko la usajili ni euro milioni 80.

HABARI MICHEZO



# WENGER

## ASHANGAA KELELE USAJILI WA POGBA, SANCHO

**PARIS, Ufaransa**

ARSENE Wenger ameonyeshwa kushangazwa na namna Jadon Sancho na Paul Pogba wanavyopamba kurasa za magazeti kwa muda mrefu kuhusu usajili wao.

Pogba kwa sasa yupo Manchester United, lakini jina lake kwa muda mrefu, tena hadharani limekuwa likihusishwa na Real Madrid.

Kwa upande wa Sancho, amekuwa akihusishwa pia na dili la fedha nyingi na klabu ya Ligi Kuu England, United, akiripotiwa kuwaniwa pale Old Trafford miaka kadhaa baada ya kuachana na Manchester City na kwenda kutamba Borussia Dortmund.

Wawili hao wanaweza kupishana pale Old Trafford, lakini wana mambo yanayofanana baada ya 'utoto' wao wote wote kukuzwa na klabu za England.

Pogba aligharimu fedha iliyovunja rekodi ya dunia aliporejea Old Trafford akitokea Juventus, wakati huo Mashetani Wekundu wakiwa tayari kulipa fedha nyingine nyingi kumnasa Sancho.

Na Wenger alisema sasa anaona kama usajili wao unakuzwa sana na wala haingii kabisa akilini mwake.

"Unaweza kumnunua mchezaji uliyemkuza mwenyewe kwa fedha nyingi," alihoji Wenger akinukuliwa na Sky Sport.

"Sidhani kama thamani yao ni kubwa kiasi hicho, wanakuzwa sana na kila wakati unasikia kuhusu habari za usajili wao."

## FLICK AJITOSA KUMTETEA LOEW

**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA wa Bayern Munich, Hansi Flick amemtetea Kocha wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Joachim Loew wakati huu akikoselewa vikali na wachezaji wa zamani wa timu hiyo.

Flick ameonyesha kumuunga mkono Loew na kusema kinachotokea hivi sasa ni cha kawaida tu na hapaswi kulaumiwa kwa mafanikio aliyoipa timu hiyo.

"Nadhani kinachotokea kwa sasa tayari kipo juu," Flick alisema Jumatano akinukuliwa na gazeti la Bild.

"Jogi amefanya kazi ya kupendeza kama kocha wa Timu ya Taifa ya Ujerumani na mafanikio yanajulikana wazi kabisa."

Hansi ametoa kauli hiyo siku moja baada ya Ujerumani kutoka sare ya mabao 3-3 na Uswisi katika mechi za kuwania kufuzu katika mashindano la Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Kocha huyo wa Bayern alikuwa msaidizi wa Loew wakati Ujerumani




iliposhinda taji la Kombe la Dunia la mwaka 2014 na aliwakosoa baadhi ya wachambuzi ambao alisema hawajakuwa na mpira miguuni mwao kwa miaka 25 au 30.

"Sasa wako pembeni na wanatoa jambo moja au jingine," alisema Flick alisema.

"Hali hii haifanyi soka la Ujerumani au hali kuwa nzuri."

Miongoni mwa wachezaji wa zamani ambao wamekuwa na ukosoaji ni Lothar Matthaeus, Dietmar Hamann, Olaf Thon, Bastian Schweinsteiger na Berti Vogts.



## ROMERO AOMBA KUONDOKA UNITED

**MANCHESTER, England**

GOLIKIPA, Sergio Romero ameiomba Manchester United kumwacha aondoke baada ya kushindwa kuondoka wakati wa usajili wa dirisha kubwa la kipindi cha majira ya joto lililopita.

Kipa huyo wa kimataifa wa Argentina mwenye miaka 33, alikuwa akitamani kuondoka Old Trafford, wakati Everton walipokuwa katika mazungumzo na United.

Romero alishindwa kutamba mbele ya David De Gea na sasa amerudi Dean Henderson baada ya kuwa na kiwango bora alipokuwa kwa mkopo kule Sheffield United.

Mke wa kipa huyo pia alionekana kumtaka Ole Gunnar Solskjaer kumwachia mumewe akatafute maisha sehemu nyingine kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii.

Taarifa zinadai kuwa Romero na mkewe walikasirika baada ya kugundua kuwa Everton ilikuwa tayari kulipa mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki.

Kipa huyo ameanza upya kwa sasa kutaka nafasi ya kuondoka United na inadaiwa ameomba mkataba wake kukatishwa ili kusaka maisha mapya ya kucheza sehemu nyingine.

Inaaminika kipa huyo aliyepoteza matumaini ya kucheza Old Trafford hataki hata malipo katika kusitisha mkataba wake, licha ya kulipwa pauni 1.5 milioni kwa mwaka.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI: SINA PRESHA YA KUPACHIKA MABAO

Nahodha huyo aeleza namna ambavyo anataka kuona mafanikio ya timu na si binafsi kama ilivyokuwa...

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi amesema siku hizi hana presha kubwa ya kutaka kufunga mabao kwani kipaumbele chake kikubwa ni kuhakikisha timu zake Barcelona na Argentina zinapata mafanikio.

Messi ndiye mfungaji bora wa wakati wote wa miamba wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Barca na Timu ya Taifa ya Argentina.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or aliongeza rekodi ya kufunga kwa timu ya taifa kwa kufikisha mabao 71 baada ya kuifungia Argentina wakati ikiibuka na ushindi wa goli 1-0 dhidi ya Ecuador kwenye mchezo wa kuwania tiketi ya kufuzu fainali ya Kombe la Dunia wiki iliyopita.

Lakini sasa Messi anaona kuwa kipaumbele chake ni timu kupata ushindi na sio yeye kufunga tu.

"Leo hii kufunga sio kipaumbele changu, mimi ninachotaka ni mafanikio ya timu na najaribu kucheza kwa ubora wangu wote kuipa mafanikio timu," alisema akinukuliwa na jarida la La Garganta Poderosa:

Messi ni mfungaji wa wakati wote wa Barcelona akiwa na jumla ya mabao 635, akiwa ameanza kuichezea klabu hiyo mwaka 2004.

Kati ya mabao hayo, 445 amefunga kwenye LaLiga - ambapo anafuatiwa na nyota wa zamani wa Real Madrid, Cristiano Ronaldo aliyefunga mabao 311.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 33 pia amefunga mabao 115 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, mabao 53 kwenye Copa del Rey, 14 kwenye Supercopa de Espana, matatu kwenye UEFA Super na matano kwenye klabu bingwa ya duniani.

Tangu alipoanza kucheza dhidi ya Espanyol miaka 16 iliyopita, Messi ameshinda mataji 10 ya LaLiga, sita ya Copa del Rey na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Msimu wa 2020-21, Messi ana bao moja katika mechi tatu za LaLiga - akiwa chini ya kocha mpya, Ronald Koeman.

## KWA UFUPI

**CHELSEA ILIMTAKA MESSI**
CHELSEA walikuwa tayari kumlipa mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, mshahara wa pauni milioni moja kwa wiki kwa uhamisho wenye thamani ya pauni milioni 225 mwaka 2014. ***(Sky Sports)***

**JUVE YAMTAKA MBAPPE**
JUVENTUS wanapanga uhamisho wa pauni milioni 360 wa kumnasa mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 21, huku klabu hiyo ya Serie A inaweza kumpeleka, Cristiano Ronaldo upande wa pili. ***(Mirror)***

**DORTMUND: SANCHO HAUZWI**
KLABU ya Borussia Dortmund haina mpango wa kumuuza winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 21, katika dirisha dogo la usajili la Januari, ambaye alihusishwa na Manchester United katika majira ya joto. ***(Sport Bild, via Mail)***

**WILSON KUTUA CARDIFF**
TIMU ya Cardiff City imekubali kumsajili winga wa Liverpool, Harry Wilson kwa mkopo, huku klabu za Derby County na Nottingham Forest zikiwa pia zinamwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Football Insider)***

**TORRES ANUKIA ARSENAL**
ARSENAL inataka kuipiku Manchester United katika mbio za kumsajili mlinzi wa Villarreal, Pau Torres mwenye umri wa miaka 23, kwa kitita cha pauni milioni 35 ifikapo Januari, mwakani. ***(Express)***

**BOLASIE MAMBO SAFI**
TIMU ya Middlesbrough inajaribu kukamilisha usajili wa winga, Yannick Bolasie mwenye umri wa miaka 31, kwa mkopo kutoka Everton. ***(Sky Sports)***

**RODON ANUKIA SPURS**
KLABU ya Daraja la Kwanza ya England, Swansea City inataka pauni milioni 18 kutoka Tottenham kwa ajili ya kumuuza beki wake wa kati raia wa Wales, Joe Rodon, mwenye umri wa miaka 22. ***(Telegraph)***

**BRUNO, SOLSKJAER SAFI**
KIUNGO wa Manchester United, Bruno Fernandes mwenye umri wa miaka 26, amekana kumnyooshea kidole Kocha Ole Gunnar Solskjaer na wachezaji wenzake baada ya kipigo cha 6-1 kutoka kwa Tottenham kabla ya mapumziko ya kupisha mechi za kimataifa. ***(Sport TV, via Metro)***

**MORRIS SALAMA DERBY**
MMILIKI wa timu ya Derby County, Mel Morris anasema kocha, Phillip Cocu hatafukuzwa hata kama timu hiyo itafungwa mechi yake inayofuata. ***(Talksport)***

**POGBA, EDUARDO KUPISHANA**
KLABU ya Manchester United imeweka mipango ya kumsainisha kiungo wa Rennes na Ufaransa, Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 17, iwapo Mfaransa mwenzie, Paul Pogba mwenye miaka 27, ataamua kuondoka Old Trafford. ***(Sport Witness)***

**CITY YAMWANIA NICOLAS**
MANCHESTER City itajaribu tena kumsajili mlinzi wa kushoto wa Ajax na Argentina, Nicolas Tagliafico mwenye umri wa miaka 28, Januari.

## HABARI MICHEZO

# USAJILI KILI MARATHON 2020 WAANZA RASMI

**Na Mwandishi Wetu**

MCHAKATO wa usajili kwa ajili ya mbio maarufu nchini ' Kilimanjaro Premium Lager Marathon 2020' umetangazwa kuanza rasmi jana, imeelezwa.

Mbio hizo zinatarajiwa kufanyika Februari 28, mwakani Mjini Moshi, Kilimanjaro.

Mkurugenzi wa mbio hizo, John Bayo alisema kama miaka yote, kuna idadi maalumu ya washiriki inayohitajika na ikishafikiwa mchakato wa usajili huo utafungwa kwa mbio zote tatu utafungwa.

Bayo alisema wanazingatia idadi maalumu, ili kuendana na taratibu za Shirikisho la Kimataifa la Riadha (IAAF) na kuhakikisha usalama wa washiriki na upatikanaji wa huduma muhimu ikiwamo taratibu zote zinafuatwa, ili kujikinga na virusi vya Covid-19.

"Tunatoa wito kwa washiriki wote wajisajili kwa wakati na kuhakikisha wanalipia, ili wathibitishe ushiriki wao, usajili umeanza rasmi leo (jana), Ijumaa Oktoba 16, 2020 ambapo washiriki watatakiwa kujisajili kwa kupitia tovuti ya www.kilimanjaromarathon.com au raia wa Kitanzania au wageni wanaoishi Tanzania wanaweza kujisajili kwa njia ya Tigopesa," alisema Bayo. Meneja wa Bia ya Kilimanajro na Grand Malt, Irene Mutiganzi, alisema wanayo furaha kudhamini kwa mara nyingine mbio hizo ikiwa ni mwaka wa kwanza tangu mlipuko wa virusi vya Covid-19, ambapo watu wataweza kujumuika tena na kufurahi kwa kupitia michezo.

"Tunatoa wito kwa washiriki wajitokeze kwa wingi na kujisajili kwa mbio za kilomita 42 na kilomita tano kwa wakati, ili wasikose nafasi," Mutiganzi alisema.

Aliongeza kampuni yao imekuwa mdhamini mkuu wa mbio hizo tangu kuanzishwa kwake miaka 19 iliyopita.

Naye Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael, alitoa wito kwa washirki watumie Tigopesa kujisajili kwani imefanya zoezi hili kuwa rahisi ikilinganishwa na hapo awali na kuongeza kuwa wale ambao hawana laini za Tigo wanaweza kuwaomba wenzao wenye laini hizo, ili kuwafanyia usajili.

"Huu utakuwa mwaka wa sita kwa Tigo kudhamini na kushiriki katika mbio hizi maarufu na za kimataifa. Natoa wito kwa washiriki wa Tigo Kili Half Marathon wajisajili kwa kubonyeza *149*20# na kufuata maelezo na kisha kukamilisha usajili wao kwa kulipia kupitia Tigopesa kwa kuwa ni rahisi na salama," alisema Shisael.

Aliwataja wadhamini wa mbio hizo ni Bia ya Kilimanjaro (mdhamini mkuu - kilomita 42), Tigo (Half Marathon), Grand Malt (kilomita tano), Maji ya Kilimanjaro, TPC, Simba Cement, Absa Bank Tanzania, Unilever, Keys Hotel, Garda World Security na CMC Automobiles.




Kiongozi wa wasanii wa tasnia mbalimbali nchini, Steven Mengele 'Steve Nyerere' akizungumza kuhusu Kongamano la Amani linalotarajiwa kufanyika katika Viwanja vya Tanganyika Pakers, Kawe jijini, Dar es Salaam leo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba, Mlandege kupimana ubavu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wanatarajia kuwakaribisha wafalme wa soka Zanzibar, Mlandege FC katika mechi ya kirafiki itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini, Dar es Salaam.

Simba inatumia mchezo huo kujiimarisha kuelekea mchezo wake dhidi ya Tanzania Prisons utakaochezwa Oktoba 22, mwaka huu wakati Mlandege yenyewe inajiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar utakaoanza mapema mwezi ujao.

Mwenyekiti wa Mlandege, Mbaraka Himid, aliliambia gazeti hili timu yao itatumia mchezo huo pia kujijenga kuelekea mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Himid alisema wameamua kucheza mechi nyingi za kirafiki na timu za ndani na nje ya Zanzibar, ili kuwapa uzoefu wachezaji wao na vile kumpa nafasi kocha kuangalia muunganiko wa kikosi chake, ambacho kina idadi kubwa ya wachezaji wapya.

"Tunahitaji kucheza mechi nyingi zaidi na timu za nje ya Zanzibar, ili tupate uzoefu, wachezaji waweze kujiamini, itatusaidia kiufundi kuelekea mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tutakuwa imara," alisema Himid.

Kiongozi huyo alisema wachezaji wao wanajifunza mbinu mbalimbali pale wanapokutana na nyota wa mataifa mengine na wanaamini michezo hiyo ya kirafiki imewaimarisha.

Kikosi cha Mlandege chenye wachezaji 27 pamoja na viongozi sita kitarejea Unguja kesho kuendelea na maandalizi yake.

## Twiga Stars, U-17 waalikwa bondeni

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) imealikwa kushiriki katika mashindano yanayoandaliwa na Baraza la Vyama vya Soka Kusini mwa Afrika (COSAFA) yatakayofanyika kuanzia Novemba 3 hadi 14, mwaka huu, Port Elizabeth, Afrika Kusini.

Akizungumza jijini, Dar es Salaam jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Clifford Ndimbo alisema mbali na Twiga Stars, pia timu ya vijana ya wasichana wa umri chini ya miaka 17, pia imealikwa kwenye michuano hiyo.

Ndimbo alisema tayari timu hizo zilishaingia kambini ikiwa ni sehemu ya programu yake ya kujiimarisha na hivyo wataondoka kuelekea kwenye michuano hiyo wakiwa imara.

"Kwa mujibu wa taarifa kutoka COSAFA, timu zinatakiwa kufika Afrika Kusini Oktoba 31, mwaka huu, kwa upande wetu tayari maandalizi yalikuwa yameshaanza chini ya Kocha Mkuu Bakari Shime," alisema Ndimbo.

Alisema baada ya kupokea mwaliko huo, TFF inasubiri kupokea programu mpya ya kiufundi kutoka kwa Shime ikiwamo kufahamu mahitaji ya mechi za kirafiki.

Mbali na timu za Tanzania, nchi nyingine zitakazoshiriki katika mashindano hayo ni pamoja na Zambia, Zimbabwe, Namibia, Botswana, Msumbiji, Malawi na wenyeji Afrika Kusini.

## Biashara United yaihofia Coastal

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya kuanza vyema msimu huu, Kocha Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, amesema mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara, dhidi ya Coastal Union ya Tanga itakayochezwa kesho itakuwa ngumu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Baraza alisema Coastal Union ni moja ya timu zinazocheza soka la ushindani na amewaandaa wachezaji wake kutowadharau.

Baraza alisema pia wanajua mchezo huo wa ugenini utakuwa na changamoto mbalimbali, lakini wataingia uwanjani kwa tahadhari.

"Mara nyingi mechi ya ugenini huwa na ushindani tofauti na tukicheza nyumbani, tunasema tutapambana ili tupate matokeo mazuri," alisema Baraza.

Aliongeza kikosi chake kilianza mazoezi jana baada ya juzi kuwapumzisha wachezaji wake, ambao walikuwa na uchovu wa mchezo, dhidi ya Ihefu FC, ambao ulimalizika kwa kupata ushindi wa bao 1-0.


Alisema wachezaji wake wote wako fiti na wanataka kuona wanaendeleza kasi ya ushindi kwenye ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tunawaomba mashabiki waendelee kutupa ushirikiano, ili tufanye vizuri katika mchezo huo, nimeona makosa madogo madogo katika mchezo uliopita na sasa tunayafanyia kazi, hatutaki kurudia makosa," alisema kocha huyo.

# Michezo

Jumamosi Oktoba 17, 2020

Nipashe

MESSI: SINA PRESHA YA KUPACHIKA MABAO HABARI UK 22




Kocha mpya wa Yanga, Cedric Kaze (kulia), raia wa Burundi akisaini mkataba wa miaka miwili wa kuiongoza Yanga inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara. Kushoto ni mwenyekiti wa klabu hiyo, Dk. Mshindo Msolla. **PICHA: MTANDAO**

# KAZE KUISUKA YANGA KISASA

## ●●●Mrundi huyo afunguka malengo yake ni kurejesha ukubwa wa klabu hiyo...

**Na Somoe Ng'itu**

HESHIMA, hiyo ni moja ya ahadi iliyotolewa na Kocha Mkuu mpya wa Yanga Mrundi, Cedric Kaze, baada ya kusaini mkataba wa miaka miwili wa kuifundisha timu hiyo ya jijini Dar es Salaam ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kaze aliwasili nchini juzi usiku na kurithi rasmi mikoba iliyoachwa na Zlatko Krmpotic ambaye alifutwa kazi Oktoba 3, mwaka huu baada ya kile kilichoelezwa timu haikuwa ikionyesha kiwango kizuri licha ya kushinda mechi nne na kutoka sare mara moja tangu kuanza kwa msimu huu.

Akizungumza kwenye makao makuu ya klabu hiyo jijini jana, Kaze alisema kilichomleta Yanga ni kuipa mafanikio klabu hiyo na si kitu kingine.

Kaze, kocha wa zamani wa Timu za Taifa za vijana za Burundi (U-17, U-20 na U-23), alisema anafahamu Yanga ni klabu yenye historia nchini na amefurahishwa na mapokezi aliyopata kutoka kwa viongozi pamoja na mashabiki.

Alisema amefurahishwa na muundo wa klabu hiyo alivyoukuta na anaamini kwa kushirikiana vyema, watafikia malengo ambayo wanayo.

"Ni faraja kubwa sana kwangu, Yanga ina wapenzi wengi Tanzania, Afrika Mashariki na duniani, nimepata ujumbe kutoka kwa watu wengi duniani, wananipongeza, nilikuwa hata sijui kama wanaijua Yanga, naweza kusema ni klabu kubwa, mashabiki wetu wajiandae, watupe ushirikiano, najua kama tutafanya vitu vikubwa," alisema Kaze.

Kocha huyo aliwahi kufundisha katika Akademi ya Barcelona alisema hana maneno mengi ya kusema na anasubiri muda wa kuanza kazi ufike ili aonyeshe vitendo.

Alisema chini ya uongozi wake atawapa kipaumbele wachezaji kwa sababu wao ndio wenye jukumu la kupambana uwanjani kuipa timu matokeo mazuri.

"Kitu ambacho kimenileta hapa ni kurudisha kuifanyia kazi Yanga kitu ambacho nataka kufanya ni kurudisha heshima ya klabu, nimeridhishwa na mfumo wa menejimenti ya uongozi, ...nitawapa nafasi kubwa wachezaji, wao ndio watafanya kazi, watatupatia matokeo," Kaze aliongeza.

Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Simon Patrick, alisema mkataba wa Kaze uliosainiwa jana utamalizika ifikapo Oktoba 15, mwaka 2022 na ataanza kufanya kazi baada ya kupata vibali.

Alisema mchakato wa kupata vibali vya kocha huyo kufanya kazi ulianza jana baada ya kusaini mkataba huo na uongozi unaomba sapoti kutoka kwa mashabiki na wanachama wa Yanga ili kufikia malengo.

Alieleza kocha huyo ndio alikuwa chaguo la kwanza la klabu na wanaamini ujio wake utawapa mafanikio yale ambayo walikuwa wanayahitaji.

Kikosi cha Yanga kilikuwa kinaendelea na mazoezi chini ya Kocha Msaidizi, Juma Mwambusi na mechi yao ya Ligi Kuu Bara inayofuata itakuwa dhidi ya Polisi Tanzania na itachezwa Oktoba 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

## BOCCO AREJEA, KAGERE MAJANGA

**Na Saada Akida**

WAKATI nyota wawili wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, nahodha na mshambuliaji, John Bocco na kiungo, Gerson Fraga sasa wako katika uangalizi maalum ndani ya kikosi hicho ili kuhakikisha wanarejea kwenye ubora wao, straika Meddie Kagere rasmi kuikosa Yanga.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, aliiambia gazeti hili jana jioni mshambuliaji huyo amepata majeraha na atakuwa nje ya uwanja wa muda wa wiki tatu.

Manara alisema kikosi hicho kinacheza mechi ya kirafiki ili kuendelea kujiimarisha kwa sababu wanafahamu mchezo wao dhidi ya Tanzania Prisons utakuwa mgumu.

"Jumatatu tutaanza safari, tunajua mchezo utakuwa mgumu, Prisons ni timu nzuri, tunakwenda kucheza kwa heshima, ili uwe bingwa ni lazima ushinde mechi zote," alisema Manara.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema lengo la kuwapa programu maalumu nyota hao ni kuhakikisha wataporejea uwanjani, kasi yao inaanzia walipoishia.

Rweyemamu alisema mazoezi ya wachezaji hao yanasimamiwa na daktari, Yasin Gembe na ndani ya siku chache zijazo wanatarajia kupokea ripoti nzuri inayohusiana na hali zao.

"Bocco na Fraga bado wapo kwenye uangalizi maalum kutokana na majeraha wanayoyunguza, wako katika uangalizi maalumu, kwa upande wa wachezaji wengine wako fiti, wanaendelea vizuri, wanasubiri muda wa mechi ufike," alisema Rweyemamu.

Alisema kikosi chao kipo kambini kwa ajili ya maandalizi ya mechi zinazofuata huku ushindani wa kusaka namba kwenye kikosi cha kwanza ukiendelea kuonekana.

"Tunafurahi kuona kila mchezaji anapigania namba, kila mmoja anaonyesha bidii kwenye mazoezi, mchuano ni mkali, hakuna ambaye anaonekana hataki namba au ameridhika, hii inampa changamoto mwalimu," Rweyemamu alisema.

Katika kuendelea kukiimarisha kikosi chake, Wekundu wa Msimbazi hao wanatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, Mlandege leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, jijini.

Simba yenye pointi 13 itashuka kucheza mechi yake ya raundi ya sita ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Tanzania Prisons ifikapo Oktoba 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela, ulioko Sumbawanga mkoani Rukwa.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002